Thomas Schirrmacher

MUNGU

Akutaka Ujifunze, Ufanye Kazi na Upende

Schirrmacher ni Profesa wa Theolojia (katika Ethics, missions, world religions), Rais wa Martin Bucer Theological Seminary na wa Giving Hands (Mikono itoayo), ambalo ni shirika hai la kimataifa la misaada; na mmiliki wa shirika la uchapaji (Publishing House). Ameandika na kuhariri vitabu 40 na anatajwa kwenye Marquis "Who's Who in the World", katika "International Who is Who of Professionals", katika "Who is Who in der Bundesrepublik Deutschland" na katika "International Who's Who in Distance Learning". Anazo shahada zifuatazo: M.Th. (STH Basel, Switzerland), Drs. Theol. (Theologische Hogeschool, Kampen, Netherlands), Drs.Theol. (Missiology, Johannes Calvin Stichting, Kampen, Netherlands), Ph.D (Cultural Anthropology, Pacific Western University, Los Angeles), Th.D (Ethics, Whitefield Theological Seminary, Lake-land, D.D. (Honorary doctorate, Cranmer Theological House, Shreveport).

ISBN 978-9987-718-01-6 (TASCM)
ISBN 978-3-928936-18-7 (RVB)

TASCM RVB INTERNATIONAL

Thomas Schirrmacher MUNGU Akutaka Ujifunze, Ufanye Kazi na Upende

TASCM | RVB

TASCM | RVB

MUNGU

Akutaka Ujifunze, Ufanye Kazi na Upende

Thomas Schirrmacher

Thomas Schirrmacher

MUNGU

Akutaka Ujifunze,
Ufanye Kazi
na Upende

RVB International
Volume 18

1	Thomas Schirrmacher:	GOD Wants You to Learn Labor and Love
2	Thomas Schirrmacher:	Legends About the Galileo-Affair
3	Thomas Schirrmacher:	World Mission – Heart of Christianity
4	Thomas Schirrmacher:	Law or Spirit – an alternative View of Galatians
5	Thomas Schirrmacher:	Human Rights Threatened in Europe
6	Thomas Schirrmacher:	Be keen to get going – William Carey's Theology
7	Thomas Schirrmacher:	Love is the Fulfillment of the Law
8	Thomas Schirrmacher:	Studies in Church Leadership
9	Monte Wilson:	The Most Important Rule for Living
10	Monte Wilson:	Principles of Success in Business
11	Th. Schirrmacher (Ed.):	A Life of Transformation – From Politician to Good Samaritan – A Festschrift for Colonel Doner
12	Thomas Schirrmacher:	DIOS Quiere Que tu Aprendas, Trabajes y Ames
13	Christine Schirrmacher:	La Vision Islamica de Importantes Enseñanzas Cristianas
14	Thomas Schirrmacher:	Sheria au Roho
15	Thomas Schirrmacher:	Upendo ni Utimilifu wa Sheria
16	Thomas Schirrmacher:	Mateso ya Wakristo Yanatuhusu Sisi Sote
17	Monte Wilson:	Sheria Muhimu Zaidi katika Kuishi
18	Thomas Schirrmacher:	Mungu Akutaka Ujifunze, Ufanye kazi, na Upende
19	Christine Schirrmacher:	Mtazamo wa Kiislamu juu ya Mafundisho Makuu ya Kikristo
20	Thomas Schirrmacher:	Tumaini kwa Afrika
21	Thomas Schirrmacher:	Mafunzo Yahusuyo Uongozi wa Kanisa

Thomas Schirrmacher

MUNGU

Akutaka Ujifunze, Ufanye kazi, na Upende

Kimetafsiriwa na Jacob M. Njagi

Kimehaririwa na Emmanuel E. Buganga

TASCM | RVB International

Bibliographic information published by the Deutsche Nationalbibliothek

The Deutsche Nationalbibliothek lists this publication in the Deutsche Nationalbibliografie; detailed bibliographic data are available in the Internet at http://dnb.d-nb.de

ISBN 978-3-928936-18-7

© Copyright 1998, 2011 by
Reformatorischer Verlag Beese
www.rvbeese.de / info@rvbeese.de
Printed in Germany

ISBN 978-9987-718-01-6

© Kwa Toleo la Kiswahili, 2011
Trans-Africa Swahili Christian Ministries
P.O. Box 772,
Mwanza, Tanzania

Toleo la Kwanza, 2011 Nakala 2,000

Maandiko Matakatifu:
The Holy Bible in Kiswahili
Union Version, 1994

Mistari ya Biblia iliyokolezwa ni tafsiri ya mwandishi mwenyewe kutoka katika Maandiko Matakatifu asilia ya Kigriki.

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kuiga, kunakili, kutafsiri, kupiga chapa, kurudufu au kutoa kitabu hiki kwa njia yoyote ile bila idhini ya Trans-Africa Swahili Christian Ministries, Idara ya Maandiko.

Kimepigwa Chapa na: Inland Press, P.O. Box 125, Mwanza, Tanzania (East Africa) TEL. +255 28 2560175 inlandpress@yahoo.com

Yaliyomo

Mungu Akutaka Ujifunze

Yesu kama Mwalimu Mkuu 7

Mungu Akutaka Ufanye Kazi

Utatu na Kazi 17

Mungu Akutaka Upende

Upendo ni Utimilifu wa Sheria: Pasipo Sheria Upendo Hufa 37

Mungu Akutaka Usaidie

Jukumu la Kijamii katika Kanisa la Agano Jipya Kulingana na Matendo ya Mitume 6 51

Mungu Akutaka Uende

Sababu za Kibiblia Kuhusu Umisheni wa Kiinjili: Hoja 31 55

Kiambatanisho:

Rushwa na Ufisadi 71

Habari Kuhusu Mwandishi

Mwandishi 75

Mungu Akutaka Ujifunze

Yesu kama Mwalimu Mkuu

Katika Agano la Kale, neno 'mfuasi' au 'mwanafunzi' huwa linatumika kwa kutambulisha mtu ambaye anamwamini Mungu. "**Bwana Mungu amenipa sikio la wenye elimu … Huniamsha asubuhi kwa asubuhi, huliamsha sikio langu kusikia kama wenye elimu**" (Isa. 50:4-5). Neno 'mfuasi' limetokana na neno la Kilatini 'discipulus' na linamaanisha 'mwanafunzi'. Agano Jipya, kwanza kabisa linatumia neno 'mathetes' ili kutambulisha mitume kumi na wawili (likianza na Yoh. 2:2 na kwa jumla katika injili hii) na kisha kuelezea wafuasi wote wa Yesu (Luka 6:17, Matendo 9:25). Agizo Kuu, ambalo pia hutumia neno hili, kwa uwazi huongea kuhusu mafundisho na kufanya yale ambayo watu wamejifunza, "mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi … na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi …" (Mat. 28:18-20). Wakristo ni wanafunzi ambao hawaachi kusoma, hii ni sifa ya kielelezo halisi cha hekima. Kadri mtu anapojua zaidi na zaidi, ndivyo mtu anavyoendelea kujua zaidi kwamba ni machache anayojua na kwamba kuna mengi yanahitajika kusomwa, "… Kumcha BWANA ni mwanzo wa hekima, na kumjua Mtakatifu ni ufahamu" (Mith. 9:8-10).

Mfano ulio mzuri zaidi wa umuhimu wa ufundishaji na wa elimu ni ule ufundishaji wa mitume kumi na wawili, ambao ulijengwa juu ya mpango wa kielimu wa kina ambao unaweza kutajwa hapa kwa muhtasari tu. Kueleza kinaganaga zaidi kutahitaji habari kuhusu elimu ya mambo yafuatanayo ambayo Yesu aliyamaliza kwa muda wa miaka mitatu na maelezo kuhusu tabia yake akiwa katika ushauri wa mtu mmoja mmoja au wa kikundi.[1] Kwa kila hali, mpango wake ulishikamanisha mafundisho na maisha, maisha ya kila siku na hotuba, mafundisho na ushauri kwa mtu binafsi, ukileta matokeo ya elimu jumuishi. Katika ulimwengu huu kila mwanafunzi anapaswa kujua na kuelewa kile mwalimu wake anachokijua. Lawrence O. Richards[2] anataja maelezo ya Yesu kwa wanafunzi wake, "Mwanafunzi hawi mkuu kuliko mwalimu wake, lakini kila mtu ambaye

---

1 Hata hivyo somo bora kabisa ni lile la A. B. Bruce, *The Training of the Twelve*, Grand Rapids: Kregel Publ., 1971 (Lilichapishwa mara ya kwanza mwaka 1894)

2 Tazama Lawrence O. Richards, *A Theology of Christian Education*, Grand Rapids: Zondervan, 1975, Tazama pia Lawrence O. Richards, *A Theology of Church Leadership*, Grand Rapids: Zondervan, 1979, na Lawrence O. Richards, *A Theology of Personal Ministry*, Grand Rapids: Zondervan, 1981

amefunzwa vema atakuwa sawa na mwalimu wake" (Luka 6:40). "Mwanafunzi hampiti mwalimu wake, wala mtumwa kumpita bwana wake. Yamtosha mwanafunzi kuwa kama mwalimu wake, na mtumwa kuwa kama bwana wake" (Mat. 10:24-25). Alipomaliza kuwaosha wanafunzi wake miguu, akawaambia, "Kwa kuwa nimewapa kielelezo; ili kama mimi nilivyowatendea, nanyi mtende vivyo. Amin, amin, nawaambia ninyi, Mtumwa si mkuu kuliko bwana wake; wala mtume si mkuu kuliko yeye aliyempeleka" (Yoh. 13:15-16). Richards anafikia hitimisho, "Elimu nyingi huhusikana na kusaidia watu kujua yale ambayo walimu wao wanayajua, elimu ya Kikristo huhusika katika kusaidia watu kuwa vile walimu wao walivyo."[3]

Wale kumi na wawili tayari walikuwa wameshasikia Yesu akihubiri kabla ya kuongoka kwao. Kwanza, wale mitume kumi na wawili wakawa wafuasi wa jumla wa Yesu. Ni mpaka hapo baadaye ndipo walipoteuliwa kutoka katika kikundi kikubwa cha watu na kuwa mitume. (Mifano ya kuitwa kwa jumla ni kuitwa kwa Petro katika Yohana 1:35-42 na Luka 5:1-11; kuitwa kwa Mlawi/Mathayo katika Mat. 9:9-13, Marko 2:13-17 na Luka 5:27-32. Linganisha kuitwa kwa wale wanafunzi wengine katika Mathayo 4:18-22 na Marko 1:16-20).

Injili zote tatu zenye kufanana hufafanua kuhusu wito wa kipekee wa wale wanafunzi Kumi na Wawili, pamoja na orodha kamili ya majina yao (Mat. 10:1-4, Marko 3:13-17, Luka 6:12-16). Acha tuangalie matukio matatu. "**Akapanda mlimani, akawaita aliowataka mwenyewe; wakamwendea. Kisha akachagua watu kumi na wawili, ili wapate kuwa pamoja naye, na kwamba awatume kuhubiri, na wawe na amri ya kuponya magonjwa na kutoa mapepo**" (Marko 3:13-16. Orodha ya majina inafuata katika mistari ya 16-19); "**Na akiisha kuwaita wanafunzi wake kumi na wawili, akawapa amri juu ya pepo wachafu, wawatoe, na kuponya aina zote za magonjwa na udhaifu wa kila aina**" (Mat. 10:1. Orodha inafuata katika mistari ya 2-4). Katika Luka 6:12, Yesu anasali usiku mzima, kisha anawaita wanafunzi wake na kuchagua kumi na wawili, "**ambao pia aliwaita mitume**" (Luka 6:13. Orodha ya majina inafuata katika mistari ya 14-16). Lazima Yesu alikuwa na wafuasi wengi zaidi, yaani wale ambao hawakuchaguliwa kuwa miongoni mwa wale mitume kumi na wawili. Tunaweza kuliona hili kwa njia tofauti. Luka 6:17 inatofautisha kati ya "makutano makubwa ya watu" na "umati wa wanafunzi", ambao pia uliwajumuisha wanawake waliofuatana na Bwana (Luka 8:2-3). Wakati Yesu alipozungumzia sifa za kuwa mwanafunzi wake, wengi waligeuka na kumwacha; lakini pia wengi, pamoja na wale

[3] Lawrence O. Richards, A Theology of Christian Education, uk. 30.

wanafunzi wake kumi na wawili, walibaki na kumfuata (Yoh. 6:66-69. Injili ya Yohana inatumia neno ‘mfuasi’ (‘mwanafunzi’) kuwaita wale kumi na wawili tu, tofauti na injili zingine).

Sababu tatu zilikuwa za muhimu katika uchaguzi wa Mitume:

1) Yesu alijiwekea yeye mwenyewe mpaka wa kuwa na idadi ndogo, kwa kuwa, kama vile baba awezavyo kuwaangalia vyema watoto wachache, Yesu angeweza kuwapa wafuasi wake wachache mafunzo bora kwa wakati maalumu.

Wale Kumi na Wawili walikuwa wamechaguliwa kuwa naye na kuyashiriki maisha yake, lakini hakuna yeyote ambaye anaweza kuyashiriki maisha yake na kikundi kikubwa cha watu. Ndoa, ambao ndio uhusiano wa karibu zaidi wa mwanadamu, imewekewa mpaka wa watu wawili pekee. Idadi ya watoto katika familia ni kubwa zaidi, lakini bado inawezekana kuishughulikia. Ufahamu wa Yesu kuwa na mpaka unaweza kuonekana pia katika vikundi vidogo zaidi vya marafiki zake, vikundi vidogo vyenye uhusiano wa karibu zaidi naye. Tena alikuwa na aliyempenda zaidi, ambaye ni Yohana, yule “mwanafunzi aliyempenda” (Yoh. 19:26; 20:2, 21:7, 20; 19:27).

Wale ndugu wawili wawili, Yakobo na Yohana, Petro na Andrea walishuhudia mambo mengi ambayo wengine hawakuyashiriki (Mat. 4:21; 10:2; Marko 1:19; 3:17; 10:35, 41; Luka 5:10; 6:14; 9:54; Matendo ya Mitume 1:13, 12:2). Hao ndugu wanne walikuwepo kwenye Marko 1:29; 13:3, wakiwa watatu bila Andrea katika Marko 5:37; 14:33 na Luka 8:51 na hasahasa wakati ule wa Kubadilika Sura kwa Yesu, Mat. 17:1-3; Marko 9:1-4; Luka 9:28-30 na baadaye, kama nguzo ya kanisa katika Wagalatia 2:9).

Vikundi vya Karibu na Yesu
Idadi kubwa (= wote), uhusiano wa kawaida * Makutano * Kundi la wanafunzi * Wanafunzi ambao walimfuata, ikijumuisha na wanawake * Wale Sabini * Wale Kumi na Wawili * Wanafunzi wanne, Petro na Andrea, Yakobo na Yohana (wale ndugu wawili wawili, au wakati mwingine walikuwa ni Petro, Yakobo na Yohana tu) * Mwanafunzi wake aliyempenda zaidi, yaani Yohana **Idadi ndogo kabisa (= mmoja), uhusiano wa karibu zaidi**

2) Yesu alichagua Kumi na Wawili, "ili wapate kuwa pamoja naye, na kwamba awatume kuhubiri, na wawe na amri ya kuponya magonjwa na kutoa mapepo". Lengo la ushirika wa kina na Yesu na hali ya kumtegemea yeye yalikuwa matayarisho ya huduma yao.

Wanafunzi hawakupaswa kubaki katika uhusiano wa karibu na Yesu tu, bali walipaswa kwenda wenyewe huko nje na kuendeleza kazi yake. Yesu alikuwa 'ametumwa' na Baba yake (Yoh. 3:16-18; 8:16, 26, 29; 12:45-49; 16:5, 28; 17:3, 8) na anatuma Roho Mtakatifu mahali pake (Yoh. 14:15-31; 16:5-11, 12-17). Anahamishia kazi yake kwa mitume. Katika Yoh. 17:18, anamwambia Baba yake, "Kama vile ulivyonituma mimi ulimwenguni, nami vivyo hivyo naliwatuma hao ulimwenguni". Katika Yohana 20:21, anawaambia wale Kumi na Wawili, "kama Baba alivyonituma mimi, mimi nami nawapeleka ninyi".

Tangu hapo mwanzo, tayari alikuwa amekusudia kuwaandaa kwa ajili ya Agizo Kuu, "mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi … na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi …" (Mathayo 28:18-20). Walipaswa kufanya jambo lile lile humu duniani ambalo alilifanya pamoja nao – kuhubiri Injili kwa watu, kuchagua wafuasi miongoni mwa kundi kubwa la walioamini, na kwa kuyashiriki maisha yao kwa kufundisha, [na] kufunza waliochaguliwa ili wawe viongozi wa kiroho.[4]

Maombi yaliyoko katika Yohana 17 hudhihirisha kwa uwazi kwamba Yesu alikuwa na kazi maalumu ambayo ilihitajika kufanywa na wale Kumi na Wawili kando na kazi ya kufa Msalabani kwa ajili ya wokovu. Katika mstari wa 4 anasema, "Mimi nimekutukuza duniani, hali nimeimaliza kazi ile uliyonipa niifanye" na anaongeza sababu, "Sasa wamejua ya kuwa yote uliyonipa yatoka kwako. Kwa kuwa maneno uliyonipa nimewapa wao; nao wakayapokea, wakajua hakika ya kuwa nalitoka kwako, wakasadiki ya kwamba wewe ndiwe uliyenituma" (Mistari ya 7-8). Yesu hakutaka tu wanafunzi wake wajue yale aliyoyajua, bali pia waishi vile alivyokuwa akiishi. Lengo la mpango wake wa mafunzo lilikuwa kwa ajili yao kufuata nyayo zake (isipokuwa tu kwa uungu wake na kwa kifo chake cha kidhabihu Msalabani). Alikuwa akirudiarudia kufundisha jambo hili kwao.

Mafunzo ya wanafunzi kwa ajili ya kazi ya umisheni, kwa Yesu mwenyewe kuishi na kufanya kazi kwa miaka kadhaa na kwa mfano halisi wa mmishenari, hayakuwa ya kukurupuka, bali yalifuata mpango wa Yesu ulio wazi. Utaratibu wa hatua kwa hatua wa mpango wake huweka jambo hili wazi. Kwanza, alihubiri yeye mwenyewe, kisha akahubiri wakati wanafunzi wake wakimtazama. Baadaye akawatuma waende kuhubiri wakati

---

[4] Tazama Robert E. Coleman, *The Master Plan of Evangelisation*, Old Tappan: Revell, 1963

akiwatazama. Baada ya hapo akawatuma katika makundi ya wawili wawili, akajadiliana pamoja nao matokeo na mwisho akawatuma peke yao[5] (akibaki pamoja nao kama Bwana Mfufuka – Mat. 28:18-20). Wale Kumi na Wawili waliendelea kufanya vile vile kwa Wakristo wengine. Mpango huu hufanya kazi vema, si tu mafunzo ya wafanyakazi wa kanisa, bali pia kwa kila aina ya elimu ambayo inajiwekea yenyewe lengo sahihi, yaani kujitegemea kuliko chini ya Mungu.

Njia Kuelekea Kujitegemea	
1)	Yesu anahubiri yeye mwenyewe
2)	Yesu anahubiri wakati wanafunzi wake wakimtazama
3)	Wanafunzi wanahubiri wakati Yesu akiwatazama
4)	Wanafunzi wanatumwa kwa kazi ya muda mfupi
5)	Wanafunzi wanatumwa kwa kazi ya kudumu.
6)	Wanafunzi wanahubiri wakati wengine wakiwatazama
7)	na kadhalika
1)	Mimi
2)	Mimi na Wewe
3)	Wewe na Mimi
4)	Jaribu peke yako, Mimi natoa maoni
5)	Uko peke yako kabisa
6)	Wewe na mwingine
7)	Mwingine na wewe
8)	na kadhalika.

3) Mpango wa Mafunzo wa Yesu kwa wanafunzi wake ulijumuisha mawanda yote ya maelekezo na maisha, nadharia na vitendo, ushauri wa mmoja mmoja na wa kikundi, shughuli ya kibinafsi na ya umma, kufanya kazi na kupumzika, maisha ya kitaaluma na ya kibinafsi. Mafundisho na Ushauri vilikuwa kitu kimoja.

Mtu anaweza kupinga kwamba kushirikishana maisha na kazi kwa kina na idadi ndogo ya watoto wa kiroho inawekewa mpaka kwa Yesu na mtume Paulo tu. Hata hivyo, 2 Timotheo 2:2 hukanusha dhana hii kwa kuamuru ufuasi kama mpango endelevu kwa kanisa na misheni: “Na mambo yale uliyoyasikia kwangu mbele ya mashahidi wengi, hayo uwakabidhi watu waaminifu watakaofaa kuwafundisha na wengine”.

[5] Huduma fupi na ya kwanza imeelezwa katita Mathayo 10:1-11, Marko 6:7-13, Luka 9:1-6. Tazama pia utumwaji wa wale Sabini katika Luka 10:1-16 na majadiliano yake pamoja nao kuhusu uzoefu waliokutana nao katika Luka 10:17-21.

Mfano wa Yesu unafanywa kuwa mpango wa lazima wa kuwafundisha wafanyakazi. Kanisa la Kristo hupanuka kupitia kwa kazi ya Wakristo waliokomaa, wenye mwelekeo wa kiroho wakiwa na vikundi vidogo vya waumini, sio kwa majaribio ya kiongozi mmoja mhusika ambaye anajaribu kufanya haki kwa watu dazani, mamia au hata maelfu kwa wakati mmoja. Ukuaji wa kweli wa kiroho na mafunzo yenye matunda hutokea pindi Wakristo waliokomaa, wenye mwelekeo wa kiroho wanapojishughulisha kwa kina na kikundi kidogo cha watoto wa kiroho, ambao wanayashiriki maisha na maelekezo yao pamoja nao mpaka pale watoto hawa wanapokuwa watu wazima ambao wanaweza kujitegemea, wao wenyewe wakiweza kuwajibika kwa ajili ya wengine. Hii ndio njia bora kabisa ya kutimiza Agizo Kuu. "mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi … na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi …" (Mathayo 28:18-20).

Fasili ya Ufuasi[6]

Kila mstari huelezea hoja kuu
– Kuwaasa wengine
– ni mchakato
– ambao kwa huo Mkristo mwenye
– maisha ambayo yanastahili kuigwa
– hujitolea mwenyewe
– kwa muda mrefu
– kwa watu wachache
– ambao wamemwamini Yesu,
– kusudi likiwa
– kusaidia
– na kuongoza
– makuzi yao hadi katika ukomavu wa kiroho
– ili waweze kuzaa matunda wao wenyewe
– katika kizazi cha tatu cha kiroho
– ambacho wanakijenga kwa kupitia ufuasi.

Tunapata msururu wa vielelezo vya kuigwa kwenye Biblia

Mifano ya Msururu wa Vielelezo vya Kuigwa kwenye Biblia

[6] Maana hii ni toleo jingine lililochukuliwa kutoka katika maana ya Allen Hadidian, *Successful Discipling*, Moody Press: Chicago, 1979. uk. 29. Kitabu hiki ni utangulizi mzuri wa ufuasi katika kanisa la mtaa.

Kumbukumbu la Torati, Yoshua, Waamuzi: Musa – Yoshua –Wazee
1 Petro 5:1-3: Yesu – Petro – wazee – wanafunzi
2 Timotheo 2:22: Paulo – Timotheo – "watu waaminifu" – "wengine pia"
1 Wathesalonike 1:6-7: Paulo – Timotheo na Silvano – Wathesalonike – Jimbo la Akaya – dunia mzima.

Kando na Yesu na wanafunzi wake Kumi na Wawili, mfano bora kabisa unaofahamika kuhusu mchakato wa ufuasi ambao unajumuisha maisha na maagizo, mafundisho na ushauri, muundo na uigaji, ni ule wa Paulo na wafanyakazi wenzake. Nyaraka kwa Wathesalonike ni ushuhuda bora kabisa kwamba si Paulo peke yake, bali pia na wenzake (Paulo, Silvano na Timotheo); wote si kwamba walihubiri Injili, bali pia waliandaliwa kuyashiriki maisha yao wenyewe na wengine (1 Thes. 2:8) kama kielelezo cha kuigwa. Kwa kawaida wote watatu walitangaza kwa maneno na kwa mafundisho. Kama sivyo, basi ni kwa namna gani wasikilizaji wao wangeelewa maana ya kielelezo chao? Nyaraka hizi zinadhihirisha jinsi Timotheo na Silvano, walivyofunzwa na Paulo kama kielelezo chao, wakawa ni vielelezo vya kuigwa kwa Wakristo huko Thesalonike ambao pia walipaswa kuwa vielelezo.

Silvano na Timotheo wanajumuishwa, kwa kuwa 1 Thes. 1:6 hutuambia, "Nanyi mkawa wafuasi wetu na wa Bwana". Wengi wameyaona maelezo haya kuwa ni ya kuchukiza. Inawezekanaje Paulo kujilinganisha na Yesu? Lakini Maandiko yenyewe yanapendekeza vielelezo vya kuigwa ili tuuige mfano wa Mungu. Je, jambo hili si la kweli? Mtoto kumwelewa Mungu hutegemea mfano wa wazazi wake, kama ni mbaya au ni mzuri. Watoto wa kiroho wanaathiriwa na mfano mzuri au mfano mbaya wa uhusiano wa wazazi wao wa kiroho na Mungu. Kila mmoja wetu ni kielelezo cha kuigwa. Si suala la kuwa mfano au kutokuwa mfano, bali mtu anaweza kuchagua tu kati ya kuwa mfano mzuri au mfano mbaya. Kila kiongozi wa kanisa na kila mwanasiasa ni mfano na anaweza kuchagua tu ni mfano upi anaotaka kuwa.

Kufuasa ni muhimu sana kwa mafunzo ya viongozi wa kiroho na wafanyakazi kanisani na katika umisheni wa kiulimwengu. Ingawa mfano wa Yesu na Paulo, au wa viongozi wa Agano la Kale, unaweza kuwa na upungufu ukiingiza katika maisha ya kisasa, lakini bado hii ndio njia bora kabisa ya kufunza na kutengeneza viongozi wa baadaye.

Nani ni Mfano Mzuri wa Kuigwa?

Vifungu vifuatavyo vyote vinatumia neno "mfano" (Kigriki: 'typos', 'hypotyposo') na maneno 'mwigaji' au 'kuiga' (Kigriki 'mimetes', 'mimetes', 'mimeistai' au 'symmimetai')

1. Mungu

Waefeso 5:1 "**Hivyo mwigeni Mungu kama watoto wapendwa;**"

2. Yesu Kristo

1 Wathesalonike 1:6, "Nanyi mkawa wafuasi wetu na wa Bwana,"

1 Wakorintho 11:1, "**Niigeni mimi, kama nami pia nimwigavyo Kristo**."

3. Mitume n.k.

Wafilipi 3:17, "**Ndugu, muungane nami kwa kufuata kielelezo changu, na mkawatazame wale waendao kwa namna ile, kama mlivyo na sisi kama kielelezo.**"

1 Wathesalonike 1:6-7, "Nanyi mkawa wafuasi wetu na wa Bwana, mkiisha kulipokea neno katika dhiki nyingi, pamoja na furaha ya Roho Mtakatifu. Hata mkawa kielelezo kwa watu wote waaminio katika Makedonia, na katika Akaya."

2 Wathesalonike 3:7, "**Kwa kuwa ninyi wenyewe mwajua jinsi iwapasavyo kutufuata sisi; kwa kuwa hatukuwa tusio na utaratibu miongoni mwenu.**"

2 Wathesalonike 3:9, "**Si kwa sababu hatuna amri, bali sisi wenyewe twajifanya kielelezo cha namna mnavyopaswa kutufuata."**

1 Wakorintho 11:1, "**Niigeni mimi, kama nami pia nimwigavyo Kristo.**"

1 Wakorintho 4:16, "**Kwa hiyo, nawasihi ninyi, niigeni mimi.**"

4. Wanaume na Wanawake katika Historia

Waebrania 6:12, "… **ili msiwe wazito, bali waigeni wale ambao kwa njia ya imani na uvumilivu huzirithi ahadi.**"

Waebrania 13:7-(8), "**Wakumbukeni wale wanaowaongoza, ambao wamelinena neno la Mungu kwenu, fuateni imani yao, mkifikiria sana matokeo ya mwenendo wao.**"

5. Baba yetu wa kiroho, aliyetumbulisha kwenye ukweli wa Biblia

1 Wakorintho 4:(14)-16, "Kwa kuwa ijapokuwa mna walimu kumi elfu katika Kristo, walakini hamna baba wengi. Maana mimi ndimi niliyewazaa katika Kristo Yesu kwa njia ya Injili. **Kwa hiyo, nawasihi ninyi, niigeni mimi.**"

6. Wazee

1 Petro 5:(1)-3, "Nawasihi wazee walio miongoni mwenu, … lichungeni kundi la Mungu … **si kama kuwa mabwana juu ya wale waliokabidhiwa kwenu, bali kuwa vielelezo kwa kundi.**"

7. Vijana wa kiume walio wa kweli

1 Timotheo 4:12, "**Mtu awaye yote asiudharau ujana wako, bali uwe kielelezo kwao waaminio, katika usemi, katika mwenendo, katika upendo, katika roho, katika imani na katika usafi.**"

8. Makanisa mengine

1 Wathesalonike 2:14, "**Kwa kuwa ninyi, ndugu, mkawa waigaji wa makanisa ya Mungu yaliyo katika Uyahudi, katika Kristo Yesu;**"

1 Wathesalonike 1:7, "**hivyo basi mkawa kielelezo kwa wote waaminio katika Makedonia na katika Akaya.**"

9. Agano la Kale na watu wake

1 Wakorintho 10:6, "**Basi, mambo haya yakawa mifano kwetu,**"

1 Wakorintho 10:11, "**Basi mambo haya yote yaliwatokea kama wao kwa vielelezo, na yakaandikwa kwa kutuonya sisi,**" (Linganisha na vielelezo vya Agano la Kale katika mistari ya 1-13).

10. Mafundisho Yafaayo

Warumi 6:17, "**… lakini mliitii kutoka mioyo mwenu aina ile ya mafundisho ambayo mliwekwa chini yake;**"

2 Timotheo 1:13 "**Shika sana kielelezo cha maneno yafaayo ambayo umeyasikia kutoka kwangu, katika imani na upendo, yaliyo katika Kristo Yesu.**"

11. Yote yaliyo mema

3 Yohana1:11, "**Mpenzi, usiige kile kilicho kiovu, bali kile kilicho chema.**"

Tito 2:7, "… katika mambo yote ukijionyesha wewe mwenyewe kuwa kielelezo cha matendo mema,"

Mungu Akutaka Ufanye Kazi

Utatu na Kazi

Tunataka kujadiliana kuhusu theolojia ya Kibiblia juu ya kazi ili kuonesha umuhimu wa mafundisho ya kidogma ya Mungu Mtatu kwa maadili yetu na kwa kujenga tena jamii.

Maadili yote ya wafanyakazi, kila maadili ya kazi, ni mwangwi wa mungu wa jamii na wa wafanyakazi wake. Nataka nitoe mifano jinsi asili ya Mungu Mtatu wa Agano la Kale na Agano Jipya inavyoakisiwa katika Sheria za kibiblia kuhusiana na kazi ya mwanadamu. Kila wakati tutakuwa pia tukiuliza kitu ambacho tunapoteza ikiwa mungu mwingine au mtazamo wa kiulimwengu ukichukua mahali pa Muumba aliyedhihirishwa katika Biblia.

> Wakati mwingi nitatumia neno mtatu badala ya Utatu. Neno la Kijerumani 'Dreieinigkeit' (utatu mmoja, utatu) huonesha vizuri sana kwamba Utatu una maadui wawili: 'mmoja' husimama kinyume na uabudu miungu wengi, 'Utatu' uko kinyume na imani ya mungu mmoja mwenye nafsi moja. Uabudu miungu wengi utaharibu imani ya Kibiblia kwa kiwango sawa na imani ya mungu mmoja asiye katika utatu. Neno la Kiingereza la Utatu halitilii mkazo jambo hili wakati 'Mtatu' hutilia mkazo. 'Mtatu' waweza kuwa mbadala ufaao kwa 'Utatu'.

Mungu ni Mungu anayefanya kazi

1. Mungu Mtatu ni Mungu anayefanya kazi. Katika Biblia, kazi ya mwanadamu ina thamani kubwa, kwa sababu humwakisi Mungu anayefanya kazi yeye mwenyewe. Mungu mtatu alikuwa akifanya kazi hata kabla ya uwepo wa wanadamu katika Uumbaji. Kwa sababu yeye ni Mungu mtatu, tena alifanya kazi katika umilele kabla ya Uumbaji kuwepo. Nafsi za Utatu zilifanya kazi kwa pamoja na kwa ajili ya kila mmoja.

Katika Biblia kila kitu kilicho kizuri hutoka kwa Utatu. Kwa sababu washirika wa Utatu huzungumza kila mmoja na mwenzake na Yesu ndiye Neno, tunaweza kuzungumza kila mtu na mwenzake. Kwa sababu Nafsi za Utatu haziishi kwa ajili yao zenyewe, bali kila moja kwa nyingine wakitegemeana, hata wanadamu wanaweza kuamriwa kufanya hivyo. Kwa sababu Nafsi za Utatu hujadiliana kila moja na nyenzake, kutokuamua mambo kibinafsi kabisa ni kanuni ya kibiblia. Katika Utatu, utii huwepo bila mtu yeyote kulazimishwa kufanya jambo: upendo na Sheria ni pacha.

Mawasiliano, upendo, kuheshimiana na kufanya kazi ili kutimiza lengo lililo nje na nafsi zetu huja kutoka kwa Utatu. Lakini Utatu ulikuwepo kabla ya dunia kuumbwa. Kwa hiyo kupenda, kuongea, kusaidia, kusikiliza na kutii vilikuwapo milele. Mungu hahitaji watu ili awepo au awe mzuri.

Kwa wafuasi wengine wengi wa dini za imani ya Mungu mmoja kama Waislamu au Wayahudi ambao hawakubali kuwa Utatu una mizizi katika Agano la Kale (Ninaongea kuhusu theolojia ya Kiyahudi, sio kuhusu mtazamo wa kibiblia juu ya Wayahudi) jambo hili ni tofauti. Ukweli ni kwamba Mungu alikuwepo hata kabla ya dunia kuumbwa. Lakini anaweza kuupenda tu Uumbaji. Hakukuwa na yeyote wa kumpenda kabla ya kumuumba yeyote. Dini zote mbili zaweza zungumzia tu kuhusu vile Mungu anavyoshugulika na Uumbaji. Wakristo wana ufunuo wa namna Mungu anavyojishughulikia kwa sababu Yeye ni Mtatu.

Kazi ya mwanadamu ina heshima kwa maana halisi ya neno. Katika Amri Kumi, kazi imeamriwa na Mungu kwa sababu zifuatazo: “Siku sita fanya kazi, utende mambo yako yote; lakini siku ya saba ni Sabato ya BWANA, Mungu wako … Maana, kwa siku sita BWANA alifanya mbingu, na nchi, na bahari, na vyote vilivyomo, akastarehe siku ya saba” (Kutoka 20:9-11). Kwa hakika Habari ya Uumbaji husema kwamba Mungu “akaacha kufanya kazi yake yote” (au “shughuli zake zote”) (Mwanzo 2:2) katika siku ya saba ya Uumbaji. Biblia kila mara huzungumzia kuhusu kazi na kujishughulisha kwa Mungu. Kwa hiyo Daudi anaomba kwa ajili ya “kazi za mikono yako” (Zab. 138:8), Sulemani anamwita Mungu “stadi wa kazi” (Mithali 8:30, vilevile Zab. 104:24) na mtunga zaburi husema: “Naam, hatasinzia wala hatalala usingizi, yeye aliye mlinzi wa Israeli” (Zab. 121:4).

Kazi na utumishi ni mojawapo ya sehemu kuu ya mfano wa Mungu. Kama mwanamume na mwanamuke waliumbwa kwa mfano na sura (Mwanzo 1:26) ya Mungu anayefanya kazi lazima wawe wanafanya kazi wao wenyewe.

Kama mungu au mamlaka ya juu ya sheria ya jamii yenyewe haifanyi kazi, hakuna heshima ya kazi. Dini ya Budha ni mfano bora kabisa. Maadili ya kazi ya kibudha yanavuviwa na mungu anayejidhihirisha katika sanamu yake mwenyewe kama aliye mnene, aliyekaa bila kazi, kwamba lengo la kila jambo si kufanya kazi bali ni “kujilaza na kusinzia”, vivyo hivyo, kuwa tajiri na mwenye kulishwa vyema. Ubudha hauna hata neno moja la “kazi” na kazi sio jambo la kuzungumziwa katika maadili yao[7]. Ubudha na Ushoshalisti una mambo mengi yanayofanana lijapo suala la

[7] Tazama Peter Gerlitz. “Buddhismus”. kr. 100-118 katika: Michael Klöcker, Udo Tworuschka (mhr.). *Ethik der Religionen – Lehre und Leben*: vol. 2: Arbeit. Kösel: Munich & Vandenhoeck & Ruprecht: Göttingen, 1985, uk. 101.

kazi na uchumi, kama vile waandishi wengi wa Kibudha walivyonena kwa uwazi[8].

Nukuu mbili za kale zitaonesha kwamba mungu wa jamii ndiye chanzo cha tathmini yake ya kazi:

> "Katika jamii ya Kigiriki kazi ilitazamwa kama ajali isiyoepukika iliyowekwa na miungu. Kuwa sawa na miungu ilimaanisha kuishi huru mbali na kazi. Katika ulimwengu wa zamani wa Mashariki, kazi ilitazamwa kama mzigo, kama vile mtumwa anavyofanya kazi kwa ajili ya miungu, ambao [miungu] walikuwa huru mbali na kazi. Lengo lilikuwa ni kujiondoa kwenye utumishi huu, mbali na kazi hii kadri iwezekanavyo. Kazi ilikuwa ni mzigo usio na heshima."[9]
>
> "Maadili ya kale yalielekeza jukumu la kazi kwa wasio huru, kwa daraja la waliokataliwa na kutengwa na jamii. Ukombozi mbali na umuhimu wa kazi kwa ajili ya mshahara tu ulitazamwa kuwa wenye thamani kwa mwanadamu. Hivyo [maadili] yaliondoa heshima ya kazi iliyoambatanishwa na mateso ya mwili."[10]

Mtazamo huu uliathiri sana theolojia ya Kikristo kama vile nukuu nyingine itakavyoonesha:

> "Thomas Aquinas alishikilia mtazamo kwamba ni uhitaji tu unaowasukuma watu kufanya kazi. Si ajabu kwamba Zama za Kati zilitazama matumizi ya kazi katika kushinda uzembe, kuudhibiti mwili na katika kujipatia mahitaji ya kuishi. Mbali ya hili, kuna tabia inayoonekana kuchukua mtazamo wa Kigiriki (kwa sehemu kubwa ni wa Ki-Aristotle) wa kutilia mkazo maisha yenye kupuuza kazi na yasiyojali maisha ya kivitendo. Hivyo ilikuwa halali kwamba wanachama wa madaraja yenye heshima na makuhani walikuwa huru mbali na shughuli za kimwili."[11]

Licha ya athari hizi za kipagani, inatubidi kukubaliana na Hermann Cremer ambaye anaongeza kwenye tathmini yake ya mtazamo wa Kigriki na Kirumi wa kazi:

---

8 Tazama rud. kr. 112-115

9 Heiner Ruschhaupt. "Bauen und Bewahren". Der Navigator Nr. 13 (Mai/Juni 1987): 2-3

10 Hermann Cremer. *Arbeit und Eigentum in christlicher Sicht*. Brunnen Verlag: Giessen, 1984. uk. 8

11 Friedrich Trzaskalik. "Katholizismus". kr. 24-41 katika: Michael Klöcker, Udo Tworuschka (mhr.). Ethik der Religionen – Lehre und Leben: vol. 2: Arbeit. op. cit. uk. 33

> "Ulikuwa ni Ukristo pekee vilevile ulio dini ya ufunuo, ulimwengu hauna budi kushukuru kwa mtazamo mwingine juu ya asili na thamani ya kazi."[12]

Alan Richardson alionesha vile Matengenezo yalivyofufua mtazamo ya Kibiblia kuhusu kazi:

> "Wanamatengenezo, Luther na Calvin, walikuwa wa kwanza kutumia maneno mwito na kazi kwa majukumu na nafasi za kila siku katika maisha ya watu. Ni muhimu kujua ya kwamba walifanya hivi katika kupinga matumizi ya lugha katika Zama za Kati ambayo yalielekeza tu wito kwenye maisha ya kimonaki. Walitaka kuharibu maadili danganyifu na kuonesha kuwa Mungu anaweza kutukuzwa pia katika ulimwengu wa siku za kazi."[13]

Misheni za Kikristo zilisafirisha maadili haya ya Kiprotestanti kwenye mabara yote. Gustav Warneck, Mjerumani ambaye ni baba wa umishenari wa Kiprotestanti aliandika:

> "… misheni za kiulimwengu za Kikristo kwa kupitia neno na kielelezo, kwamba kazi (ambayo kupitia kwa utumwa ilibeba unyanyapaa mwovu), ilikuwa na msingi wa amri ya Mungu …"[14]

Mungu ni mfanyakazi kupita wote kwa sababu yeye ndiye Mamlaka Kuu

2. Mungu Mtatu hufanya kazi kushinda mtu mwingine yeyote. Kwa hiyo, kadri mtu anavyokuwa na wajibu zaidi ndivyo anavyozidi kuwa na kazi nyngi.

Mfano wa Ubudha au mtazamo wa Kigiriki na Kirumi uliweka wazi lengo la jamii hizi kuwa kama miungu yao, ambalo ni kuwa huru mbali na kazi. Kama yule mkubwa zaidi hafanyi kazi kabisa, kazi nzito zitapatikana kwa wale walio chini tu. Kadri unavyozidi kwenda juu, ndivyo watu wengi watavyozidi kuishi kwa kufanya kazi za wengine. Unyonyaji hauepukiki katika jamii kama hii.

Katika Biblia tunaona mtazamo tofauti na huu. Tayari tumeshaona kwamba Mungu "halali wala hasinzii" (Zab. 121:4). Kwa sababu Mungu Mtatu ameshafanya na hufanya mengi kushinda mtu yeyote yule, yeye ni

---

[12] Hermann Cremer. Arbeit und Eigentum in christlicher Sicht. Brunnen Verlag: Giessen, 1984. uk. 8

[13] Alan Richardson. *Die biblische Lehre von der Arbeit*. Anker-Verlag: Frankfurt, 1953. uk. 27

[14] Gustav Warneck. *Die Stellung der evangelischen Mission zur Sklavenfrage*. C. Bertelsmann: Gütersloh, 1889. uk. 67

mfano kuwa wajibu humaanisha kazi. Je, si mtume Paulo ambaye aliandika mara mbili kuwa "nalizidi sana kufanya kazi kupita wao wote" (1 Kor. 15:10; 2 Kor. 11:23)? Huku hakukuwa kujivuna bali matokeo ya kawaida ya wajibu wake mkuu kama mtume. Kuwa mtume hakukumaanisha eti kuwa na wakati zaidi wa starehe, wafanyakazi zaidi au utajiri mkubwa, bali machozi na kazi na kulala kidogo. Hii ndio sababu ambayo Martin Luther, hapo mwanzoni mwa Matengenezo, wakati alikuwa angali anaamini katika uwezekano wa kuubadilisha Upapa, alimwandikia Papa barua akimkaripia kwamba anapaswa kufanya kazi zaidi kwa ajili ya ustawi wa Kanisa kuliko mtawa au kuhani yeyote ikiwa ni pamoja na Luther mwenyewe. Alimwuliza Papa ni kwa namna gani aweza kulala usingizi kwa amani, katika mtazamo wa uwajibikaji, wakati Kanisa la dunia nzima liko katika msukosuko. Kinyume na wajibu wake, Papa alitumia wakati mwingi kwa ajili ya kustarehe na kufanya sherehe.

Ukimpoteza Mungu mtatu, tabia ya Kikristo kwamba wajibu zaidi huleta kazi zaidi utabadilika na kufuata mtazamo wa kiyumanisti na wa kimabavu, kwamba watu walioko katika vyeo vya chini hufanya kazi kwa ajili ya watu wenye vyeo vya juu hivyo basi hawa wakubwa hawahitaji kufanya kazi wao wenyewe.[15]

Umaksi huilaumu jamii kwa unyonyaji wa daraja la chini, kwa hiyo unaonekana kuwa na mtazamo hasi kwa watu walio katika vyeo vya juu, ambao huwafanya wengine wafanye kazi wakati wao wenyewe hawafanyi kazi. Lakini Umaksi hauna fasili nyingine ya kazi. Kazi daima ni kazi ya kinyonyaji ya daraja la chini. Kama vile Umaksi ulivyo, una 'maada' na 'historia' kama miungu yake, hakuna njia yoyote ya kuepuka unyonyaji. Si ajabu serikali na jamii za kishoshalisti ni mifano mizuri ya kanuni za Kiyumanisti kwamba kadri unavyopanda juu, ndivyo unavyozidi kupunguza kazi ngumu. Si ajabu kwamba Karl Marx na Friedrich Engels kamwe hawakuwa wafanyakazi bali walikuwa waajiri wazembe. Marx mwenyewe alijichumia fedha mara moja katika kipindi cha muda mfupi sana – kama mmiliki wa gazeti la Kimaksi. Baadaye aliishi kwa kutumia pesa za Engels ambaye alikuwa tajiri kwa sababu alirithi viwanda kutoka kwa baba yake. Hakuna hata dokezo kidogo kwamba Marx au Engels waliwahi kuwa na dhamiri yenye hatia kwa kutumia fedha ambazo walizipata kutokana na kazi ngumu za wafanyakazi, au hata kama Marx alihuzunika kuhusu maisha yake ambayo yalikuwa ya kutozalisha kadri iwezekanavyo, kama hutatilia maanani baadhi ya vitabu vyake vikubwa ambayo havikuwa tayari kwa wakati wake. Konrad Löw anasema:

---

[15] Tazama sura inayohusu maadili ya kazi katika kitabu changu kiitwacho *Marxismus – Opium für das Volk?* Schwengeler Verlag: Berneck, 1990

"Kwa kulingana na nadharia yao wenyewe, Marx na Engels daima waliishi kwa fedha ambazo hawakustahili."[16]

Kwamba, katika nchi za Kikomunisti uzalishaji na kiwango cha mazao kiliendelea kupungua kadri muda ulivyoendelea, na si matokeo pekee ya mfumo wa Serikali na uongozi mbaya wa Serikali. Sababu kuu ni maadili ya waajiriwa kwa kuwa maadili ya kazi ni mwangwi wa dini ya ukosa-Mungu. Kama kazi nzito hutazamwa kama unyonyaji, ni namna gani Umaksi utawaeleza wafanyakazi kwamba jambo hili ni tofauti ikiwa mwajiri ni Serikali ya Kimaksi?

'Ubepari wa ukosa-Mungu' – kama niuitavyo, Ubepari unaokana Sheria za Mungu na hivyo kuwa dini ya Fedha – kwa haraka huifikia hali sawa na ile ya Kimaksi, Ubudha na dini nyingine. Watu wengi wa jamii ya Magharibi wana lengo la kuwa matajiri katika maana ile ya kuwa huru mbali na kazi. Kama matokeo ya tabia hii inayokua haiwezi kuonekana kwa mara moja, sababu ni kwamba maadili ya kibiblia ya kazi ya Kiprotestanti bado yanafanya kazi mahali pengi, ijapokuwa msingi wake umepotezwa. Rais, Kansela au Waziri Mkuu bado anatarajiwa kufanya kazi zaidi kupita raia wa kawaida. Asingeweza kupata kura nyingi kama angefanya kama wafalme wa Ukamilifu na zama za Mwako, ambao kwa sehemu kubwa ya muda wao walijihusisha na sherehe na starehe. (Ni Mfalme mmoja tu wa Kifaransa, aliyewapokea wanadiplomasia wakati akiwa msalani!)

Kwamba, mamlaka zaidi hutuongoza kwenye kazi zaidi, ni kanuni ya kipekee ya Kikristo kwa sababu kila mamlaka hutoka kwa Mungu, ambaye ni kielelezo kisichoshindwa kwa kila mmoja juu ya mamlaka, kwamba mamlaka humaanisha kufanya kazi kwa ajili ya mema ya wengine. Wazazi wana mamlaka juu ya watoto wao. Je, jambo hili linawapunguzia kazi? Hapana, linawafanya wafanye kazi na kuwagharimu usingizi mwingi. Ole wao wazazi ambao hutaka mamlaka bila kufanya kazi. Ole wake yule ambaye hutaka haki za mamlaka lakini sio kazi zake! Mungu hugawanya tu mamlaka pamoja na kazi ya kufanya!

Jambo hili pia ni kweli juu ya kazi kwa ujumla wake. Kazi ya wanadamu kuitiisha nchi (Mwa. 1:26-30), ilikuwa ni amri ya kufanya kazi. Bustani ya Edeni haikuwa tu shamba la kufikirika la starehe, haikuwa mahali pa paradiso ya wajinga, kama ilivyo paradiso ya Umaksi na Uislamu. Katika Uislamu mwanadamu hakufanya kazi katika paradiso,

---

[16] Imenukuliwa kutoka katika Löw. Marxismus Qellenlexikon. Kölner Universitätsverlag: Köln, 1985. uk. 321

kazi yake haikuja kwa kulaaniwa na hatakuwa akitumika mbinguni[17]. "BWANA Mungu akamtwaa huyo mtu, akamweka katika bustani ya Edeni, ailime na kuitunza" (Mwanzo 2:15). (Hapa Mungu anataja pande mbili za kazi yoyote, ambazo ni ubadilikaji na uendeleaji, kuweka sawa na kuhifadhi. Uyumanisti daima hutilia mkazo upande mmoja au mwingine, Biblia huziweka zote pamoja). Kabla ya Anguko, tunaona kazi aina mbalimbali za kazi ambazo Adamu na Hawa walipaswa kuzifanya. Walipaswa kumwagilia na kuotesha mimea (Mwa. 2:5), kujipatia dhahabu na vito vya thamani (Mwa. 2:10-13), kujipatia chakula chao (Mwa. 2:9), na kumpa jina kila mnyama (Mwa. 2:19-20). Adamu alikuwa mwanasayansi mwanabaolojia wa kwanza. Ni ajabu mno kwamba Habari ya Uumbaji husema kwamba Mungu alimpa Adamu haki ya kuwapa majina wanyama na Mungu aliyatumie yale majina ya Adamu: "kila kiumbe hai, jina alilokiita Adamu likawa ndilo jina lake" (Mwa. 2:19). Sikiliza ufupisho wa mtazamo wa kazi wa agano la Kale na wa Kiyahudi.

> Kazi "sio matokeo au adhabu ya dhambi – kulingana na mtazamo usiopingika wa wachimbuzi-tafsiri wa Kiyahudi wa Mwa. 3:17-19, ni ule ugumu wa kazi na kushindwa mara kwa mara tu ndiko kunasimama kinyume na urahisi na uhuru mbali na utunzaji uko Paradiso. Kazi ya mwili kwa ujumla haidharauliwi miongoni mwa Wayahudi kama vile ilivyokuwa miongoni Wagriki na Warumi."[18]

Wilhelm Lütgert vilevile anaandika:

> "Sio kazi yenyewe bali ni uwiano usio sawa wa kazi na mapato au matokeo na maumivu na suluba ambazo husimama katika uwiano usio sawa na matokeo, ndio matokeo ya dhambi."[19]

Hata hivyo: Kulingana na Isaya katika Milenia (tazama Isa. 65:17-25), kazi na utumishi kamwe havitakuwa bure: "Nao watajenga nyumba, watapanda mizabibu na kula matunda yake. Hawatajenga, akakaa mtu mwingine ndani yake, hawatapanda, akala mtu mwingine; … wateule wangu wataifurahia kazi ya mikono yao muda wa siku nyingi. Hawatajitaabisha kwa kazi bure …" (Isa. 65:21-23).

---

[17] Tazama Monika Tworuschka. "Islam". kr. 64-84 katika: Michael Klöcker, Udo Tworuschka (mhr.). *Ethik der Religionen – Lehre und Leben*: vol. 2: Arbeit. op. cit., kr. 67+69

[18] Johannes Wachten. "Judentum". kr. 9-23 katika: rud., uk. 10

[19] Hermann Cremer. *Arbeit und Eigentum in christlicher Sicht*. op. cit. uk. 9

Kazi ya Mungu itapokea ujira wake

Katika Biblia, kazi ina hadhi na thamani hata kama inalipwa au hailipwi. Lakini Sheria inayonukuriwa mara kwa mara na kwa wingi: "Mtenda kazi astahili ujira wake" (1 Timotheo 5:18; Luk. 10:7) ni matokeo ya hili. **Kazi si yenye thamani tu pindi inapolipwa, bali kazi hulipwa kwa sababu ni kitu chenye thamani.**

Biblia huchukulia kwa makini sana amri ya kuilipa kazi yoyote inayonekana katika Yer. 22:13, "**Ole wake yule ambaye hujenga kasri yake kwa uovu, vyumba vyake vya juu pasipo haki; akifanya watu wa taifa lake wafanye kazi bila chochote, kwa kutowalipa kwa kazi yao**".

Kwa hiyo, kazi zote hustahili malipo, lakini malipo hayo siyo lazima yawe ni fedha. Kila mtu anaweza kuamua ni malipo gani anayotaka au kukataa malipo ya kidunia. Chukua mfano wa sifa kwa mke mwema katika Mithali 31. Kazi ambayo inalipwa na ile ambayo hailipwi, moja kwa moja husimama ana kwa ana. Kazi ya mke huyu wa nyumbani imejaa thamani.

Amri ya Mungu ya kufanya kazi kwa siku sita, kama tunavyoipata katika Amri Kumi, ni amri ya jumla kwa wanaume na wanawake. Watu hawapaswi kukaa tu bila kazi, bali wafanye kazi; isipokuwa Jumapili. Kazi si tu sheria ya kimaumbile au hitaji la kimaumbile, eti kwa sababu ama sivyo tungekufa kwa njaa, bali ni utararibu ulioumbwa. Kwa hiyo, "moja ya mashitaka makali zaidi ya manabii ni dhidi ya watu matajiri (kwa mfano, Amosi 6:3-6)."[20] Unaweza kuwa tajiri lakini usiwe mzembe. Ni mapenzi ya Mungu na ametupa sisi Uumbaji wake kwa lengo hili.

Je, mfanyakazi ambaye hajaajiriwa anaweza kufanya nini? Afanye kazi, bila shaka! Ingawa hatutaki kuchukulia jambo la kukosa ajira kwa urahisi, mtu ambaye hajaajiriwa anaweza kufanya kazi za aina nyingi bila mshahara. Anaweza kusaidia familia yake, kusaidia wahitaji au kanisa lake. Ulegevu au kuwalaumu wengine si suluhisho la ukosefu wa ajira.

Je, Umaksi una cha kusema kuhusu ujira wa haki? Hakuna! Kwa mtazamo wa Marx, katika ubepari malipo yote si ya haki lakini hakuna ambaye ana haki ya kubadili jambo hili. Tofauti kati ya matengenezo ya kijamaa ya Kikristo na mapinduzi ya Kimaksi inakuwa bayana katika utafiti wa Marx uitwao 'Critique of the Declaration of Gotha' (Ukinzani wa Azimio la Gotha), ulioandikwa wakati akiwa mzee na akichangia mawazo katika jukwaa la Chama cha Kijamii na Kidemokrasia cha Ujerumani. Takwa la hiki Chama cha Kisoshalisti ni "kwamba matokeo yote ya kazi yanafaa kuwa, kwa mujibu wa haki sawa, ya kila mtu kwa kulingana na hitaji lake wakati huo huo kila mmoja akiwa na jukumu la

---

[20] Alan Richardson. *Die biblische Lehre von der Arbeit*. op. cit. uk. 16

kufanya kazi”[21] – likiwa limejaa mikanganyiko – linakataliwa kabisa na Marx, kwa sababu bado limejikita katika dhana ya sheria na haki. Marx anaandika: “Ni haki ya ukosefu wa usawa[22] juu ya yale yaliyomo kama haki yote ilivyo”. Anaendelea: “Kwa kanuni, haki sawa hapa bado ni haki ya mabwanyenye …”[23] Hili haliwezi kukubaliwa kwa sababu bado “kimya kimya linakubali tofauti ya vipawa vya mtu binafsi na kwa hiyo utendaji kazi tofauti wa wafanyakazi kama upendeleo wa asili”.[24]

Marxi alisoma sheria katika Chuo Kikuu cha Bonn na kwa hiyo alifahamu kile alichokuwa akizungumza. Hakutaka kubadilisha msimamo wowote wa kisheria bali kungojea unabii wake utimie na kuwa wa ukweli. Unabii wake ulihitimisha kwamba jamii ya Kikomunisti haitaleta matokeo ya haraka:

> “Lakini malalamiko haya hayawezi kuepukwa katika hatua ya kwanza ya jamii ya Kikomunisti kama ambavyo imetokea kwa jamii ya kibepari baada ya muda mrefu wa machungu ya kazi.”[25]

(Kwa Kijerumani, hapa Marx anazungumza katika unabii timilifu, kama manabii wa Agano la Kale walivyofanya mara kwa mara!) Engels anaelezea hili kwa uwazi zaidi:

> “Tunatupilia mbali jaribio lolote la kuweka wazi mbele ya hakimu mkorofi, kwamba Marx kamwe hakudai ‘haki kwa mazao yote ya kazi’ na kwamba kamwe hazungumzii takwa lolote la kisheria la aina yoyote katika maandishi yake yoyote ya nadharia.”[26]

Anaendelea:

> “Marx anagundua historia isiyokwepeka, ambayo ni haki ya mtumwa na mkuu wa hapo zamani, bwana wa kikabaila wa Zama za Kati n.k., kama nyenzo ya maendeleo ya binadamu katika wakati fulani wa kihistoria. Kwa wakati mwingine anakubaliana na haki ya unyonyaji …”[27]

---

21 Ursula Schulz (mhr.). *Die deutsche Arbeiterbewegung 1848-1919 in Augenzeugenberichten*. Dtv: Munich, 1981[3]. uk. 200

22 Karl Marx. Friedrich Engels. Werke. Kit. 42. Dietz Verlag: Berlin. 1956k. Kit. 19. uk. 20

23 Rud.

24 Rud. uk. 21

25 Rud.

26 Rud. Kit. 21. uk. 501

27 Rud.; soma ukurasa wote

Hakuna mtu yeyote ambaye amewasoma Marxi na Engels hufikiria kuwa Marxi alikuwa akipigania haki za wafanyakazi. Kwa mujibu wao wote wawili, mfanyakazi ni lazima ajitiishe chini ya mahitaji ya kihistoria na kungojea hadi vita vya matabaka vifikiapo hatua inayofuata. Haki haiombwi. Umaksi huulaumu Ukristo kwa kuwatuliza watu kwa matumaini ya mbinguni, kwa sababu yeye haelewi kwamba tumaini hili ndilo msingi wa mabadiliko hapa duniani na kwa haki yoyote ile. Lakini Marx mwenyewe anawatuliza watu kwa maono yake ya kinabii. Lakini Paradiso itakuja tu baada ya Umaksi wa leo kufa. Hakuna mfuasi wa Umaksi yeyote ambaye amekwishapata chochote kwa tumaini lake hilo, ama hapa duniani au huko Mbinguni.

Kwa mfano, Marx alipinga sheria za Uingereza na za Ujerumani zilizokuwa kinyume na kazi za watoto zilizo kama za kitumwa. Alisema sheria kama hizi zilikuwa za "msisimko"[28], kwa sababu hazikubaliani na Ubepari na viwanda vikubwa – historia ilimhukumu kuwa amekosea – na kwa sababu ilidunisha maendeleo ya hatua ya mwisho ya Ubepari. Marx hakutaka kuwasaidia wanyonge lakini alitaka kuona unabii wake ukitimia. Marx hakusema lolote juu ya watoto wanyonywao, lakini aliona tu tatizo kwamba Umaksi ungepoteza nguvu kubwa ya mapinduzi kama watoto wangekuzwa katika mazingira bora.[29]

Kutojali kusikokuwa na mipaka kwa haki za wafanyakazi na kila kitendo kuelekea uhusiano wa haki kati ya waajiri na waajiriwa kunaweza kuthibitishwa na nukuu nyingi kutoka kwa Marx na Engels[30]. Marx aliandika hivi kuhusu Bunge la Ujerumani:

> "Kwa sababu mnaweza kutumia bunge kama njia ya mabishano, kamwe hamtaweza kubishana ndani ya bunge kwa kitu kinachokubalika na fikra au kwa kitu ambacho kina maslahi ya moja kwa moja kwa wafanyakazi."[31]

---

[28] Rud. uk. 32 ("Allgemeines Verbot der Kinderarbeit ist unverträglich mit der Existenz der großen Industrie und daher leerer frommer Wunsch. Durchführung desselben – wenn möglich – wäre reaktionär, da, bei strenger Regelung der Arbeitszeit nach den verschiedenen Altersstufen und sonstigen Vorsichtsmaßregeln zum Schutze der Kinder, frühzeitige Verbindung produktiver Arbeit mit Unterricht eines der mächtigen Umwandlungsmittel der heutigen Gesellschaft ist.").

[29] Tunataka kuonesha msimamo wa Maksi, siyo kujadili ufanyaji kazi wa watoto au haki ya Serikali kuirekebisha.

[30] Konrad Löw. *Marxismus Qellenlexikon*. Kölner Universitätsverlag: Köln, 1985. kr. 221-222

[31] Karl Marx. Friedrich Engels. *Werke*. op. cit. Kit. 32. uk. 360

Umaksi una tatizo sawa na lile la Ubepari usio na Mungu. Vyote hutoa wito wa kazi ya haki, lakini havina sheria ya kulinda haki hii. Wakati Umaksi haukubali haki yoyote kufanywa kuwa sheria, marafiki zake wa Kibepari hujaribu kuweka mitazamo yao kuwa sheria. Lakini dini ya "Mali" inaweza tu kutambua haki katika hali ya fedha. Haki kila wakati humaanisha kupata pesa zaidi kwa kufanya kazi kidogo. Wanasahau kuwa haki inaweza tu kuwa haki, kama inaratibu kila sehemu ya maisha, sio mambo ya fedha tu.

Kazi ya Mungu ni kazi kwa ajili ya Mungu

Kama Mungu asingefanya kazi kwa ajili yetu, tusingeweza kufanya kazi kabisa. Ingawa binadamu aliumbwa kufanya kazi na asiwe mzembe, amri ya kufanya kazi ni sehemu pekee ya amri ya kumtumikia Mungu. Katika Biblia, daima kazi ya mwanadamu ina mipaka. Mbali na hadhi yake, kamwe kazi si jukumu la kwanza, bali daima ni la pili. *Kamwe kazi si mwisho wenyewe! Ni mtazamo wa kipekee wa Kikristo wa kuunganisha utukuzaji mkuu kabisa wa kazi kama kitu kisichofaa kama haifanyiki katika taswira ya Mungu, pamoja na mipaka ya kazi, hivyo basi mwanadamu asitawaliwe kabisa na kazi, bali aiweke kazi chini ya mkono wake na chini ya utawala wa Mungu.* Ni pale tu utakapoona pande hizi mbili kwa wakati mmoja ndipo utakapoelewa matokeo yafaayo ya maadili ya kazi ya Kibiblia.

Hii ndio maana ya Sabato. Sabato humkumbusha mwanadamu kuwa, anaweza kufanya kazi tu kwa "siku sita za kazi" (Eze. 46:1), kwa sababu Mwumba wake hufanya kazi kwa ajili yake na amempa mwanadamu Uumbaji kwa matumizi yake. Mungu pia anafahamu ya kwamba kufanya kazi mchana na usiku bila kupumzika si jambo zuri kwa mwanadamu.

Tayari tulishazungumzia dini zenye mtazamo duni juu kufanya kazi ngumu. Lakini pia kuna dini ambazo zina mtazamo wa juu sana ambazo zinakosa marekebisho ya maadili ya kazi kwa siku nzima bila kupumzika. Umoja wa wanasheria wa Japani husema kwamba katika nchi ya Ujapani kuna watu 10,000 hufa kila mwaka kwa kufanya kazi zaidi[32]. 'Kifo kinachosababishwa na kufanya kazi zaidi' kinakubaliwa na Waziri wa Kazi wa Japani kama chanzo rasmi cha kifo. Kuna neno maalumu la kifo kutokana na kufanya kazi kupita kiasi kwa lugha ya Kijapani, 'karoshi'. Kifo kutokana na kufanya kazi kupita kiasi inasemekana ni matokeo ya wingi mkubwa wa kazi ya muda wa ziada na kukosekana kwa nyakati za maburudiko. Mara nyingi "nyumba huwa mahali pa kulala tu"[33].

---

[32] D. P. "Zu Tode gearbeitet". Der Kassenarzt No. 12/1991, uk. 32

[33] Rud.

Siku ya saba bila kazi huwakumbusha wanadamu kwamba bila Mungu wasingeweza kufanya kazi kabisa. “BWANA asipoijenga nyumba waijengao wafanya kazi bure. BWANA asipoulinda mji yeye aulindaye akesha bure. Kazi yenu ni bure, mnaoamka mapema, nakukawia kwenda kulala, na kula chakula cha taabu; **yeye huwapa usingizi wale awapendao.**” (Zab. 127:1-2). Mithali 10:22 husema kwa kifupi zaidi: “Baraka ya BWANA hutajirisha, wala hachanganyi huzuni nayo” (pia angalia Mat. 6:24-34). Na Yesu anawaambia wanafunzi wake: “maana pasipo mimi hamwezi kufanya neno lolote” (Yoh. 15:5).

Wachanganuzi wa Maandiko wa kiuzamo (kipayatisti) na wale wa kiliberali kwa pamoja huiona mistari hii kama yenye kurejea kwenye kazi za kidini, baadhi ya baraka za kiroho au baadhi ya nyumba za kufikirika. Mpayatisti huamini kuwa hawezi kufanya uinjilisti bila Yesu au hawezi kulikuza kanisa lake bila Yesu. Bila shaka jambo hili ni kweli, lakini vifungu ambavyo vimenukuliwa vinahusu kazi zote, kila kitu afanyacho binadamu na bila shaka kazi yake ya kila siku. Kulingana na Kutoka 31:2-6 na 35:31, wahandisi wangeweza kujenga hema zuri, kwa sababu Mungu alikuwa amewapatia Roho wake mwenye vipawa vya ubunifu wao.

Kwa hiyo kuwa mwenye shukrani ni sehemu muhimu sana ya kazi yoyote. “Isa. 28:23-29 husema kwamba matokeo ya wakulima ya kulima, kupanda, kuivisha, kufyeka, kupura na kuoka mkate hurejea kwenye mafundisho ya Mungu”[34]: “Kwa maana Mungu wake anamwagiza vizuri na kumfundisha.” (Isa. 28:26)[35].

Kuna njia nyingine zilizowekwa za kueleza ukweli ya kwamba kazi si kila kitu, na kwamba mtu anahitaji kumshukuru Mungu kwa ajili ya uwezo wa kufanya kazi. Fungu la kumi huja moja kwa moja kutoka kwenye kile mtu anachopata. Fungu la kumi si kipande tu cha mapato bali ni *zao la kwanza* la kazi zetu kudhihirisha ya kwamba Mungu na kushukuru huanza kwanza kabla ya kutumia matokeo ya kazi zetu. Jambo hili ni sawa na lile la utoaji dhabihu. Gustav Friedrich Oehler ameonesha kwamba mimea yote na wanyama wote kwa ajili ya dhabihu walikuwa ni “chakula cha kawaida ambacho watu wangeweza kujipatia kupitia kazi yao ya kawaida”[36]. Hili laweza kuonekana katika kumbukumbu ya kwanza ya dhabihu katika historia iliyotolewa na Abeli na Kaini ambao wote walitoa mazao yao ya kwanza ya utaalamu wao. Jambo hili pia huonesha uhusiano wa karibu kati ya kazi za kila siku, huduma na utoaji shukrani kwa Mungu.

---

34 Alan Richardson. *Die biblische Lehre von der Arbeit*. op. cit. uk. 15

35 Tazama maelezo katika muktadha.

36 Gustav Friedrich Oehler. *Theologie des Alten Testaments*. J. F. Steinkopf: Stuttgart, 1891[3]. uk. 437

Hakuna kazi ifanywayo kwa ajili ya mtu au familia yake au mwajiri wake bali katika uchambuzi wa mwisho ni kwa Mwajiri Mkuu,[37] Mungu Mwenyewe. Hivyo Paulo asema: "Na kila mfanyalo, kwa neno au kwa tendo, fanyeni yote katika jina la Bwana Yesu, mkimshukuru Mungu Baba kwa yeye" (Kol. 3:17). Tena hili haliwezi kupunguzwa kuwa katika mtazamo wa kiuzamo. Hili linathibitishwa na moja ya mistari ifuatayo iliyoandikwa kwa watumwa, lakini bado ni sahihi kwa kila mmoja: "lolote mfanyalo, lifanyeni kwa moyo, kama kwa Bwana, wala si kwa wanadamu, mkijua ya kuwa mtapokea kwa Bwana ujira wa urithi. Mnamtumikia Bwana **Yesu**" (Kol. 3:23-24).

> "Heshima ya kazi haitokani na kile ufanyacho bali kwa nini unakifanya. Kwa sababu ya agizo la utumishi lililotolewa na Mungu na tabia ya utumishi katika kazi kuelekea kwa jirani yako, kazi yenye ufundi kidogo kabisa ni yenye thamani sawa na kazi 'itumiayo akili sana'".[38]

Watu wengi hulilaumu Agano Jipya kwa sababu huwaamuru watumwa kuwa wafanyakazi wazuri (kwa mfano, Tito 2:9-11; Efe. 6:5-9; Kol. 3:22-4,1; 1 Tim 6:1-2; 1 Pet. 2:18-25; 1 Kor. 7:21-24). Tayari tumekwishasikia sababu kwa ajili ya hilo. Watumwa hufanya kazi kwa ajili ya Mungu, si kwa ajili ya mwajiri wake. Huu ndio uhuru halisi! "Ninyi watumwa, watiini hao ambao kwa mwili ni bwana zenu, katika mambo yote, si kwa utumwa wa macho, kama wajipendekezao kwa wanadamu, bali kwa unyofu wa moyo, mkimcha Bwana" (Kol. 3:22). Hakuna kazi chafu au kazi mbaya katika Biblia, isipokuwa zile kazi na taaluma ambazo zimekatazwa moja kwa moja na Mungu kama vile umalaya. Mwajiri mwanadamu si mtoaji halisi wa mishahara, bali [mlipaji halisi] ni Mwajiri mkuu wa Uumbaji. *Ni kwa sababu tu Mungu, aliye Mwajiri mkuu, hutupatia mshahara wa haki, ni lazima waajiri wanadamu wafanye vivyo hivyo.*

Paulo yule yule anayetuambia watumwa wawe wafanyakazi wazuri, anawaandikia: "Kila mtu na akae katika hali ileile ambayo alikuwa nayo alipoitwa. Je! Uliitwa u mtumwa? Usione ni vibaya *lakini kama ukiweza kuwa huru, afadhali kuutumia.* Kwa maana yeye aliyeitwa katika Bwana hali ya utumwa, ni huru wa Bwana. Hivyo yeye aliyeitwa hali ya uhuru, ni mtumwa wa Kristo. Mliumbwa kwa thamani; msiwe watumwa wa

---

[37] Kwa Kijerumani 'mwajiri' ['Arbeitgeber'] humaanisha 'mtoa kazi', 'yule atoaye kazi'. Kwa Kijerumani tunaweza kusema kwamba Mungu ni 'Arbeitgeber' mkuu, yeye aliye mkuu sana mwenye kutoa kazi kwa wanadamu.

[38] Emil Brunner. *Das Gebot und die Ordnungen*. Zwingli Verlag: Zürich, 1939[4]. uk. 373

wanadamu" (1 Kor. 7:20-23). Katika waraka wa Paulo kwa Filemoni Paulo anajishughulisha na kuachiwa kwa watumwa. Je, huku ni kupingana? Hapana, kwa sababu Paulo anasema: "Lakini kama ukiweza kuwa huru, afadhali kuutumia". Lakini mtumwa hahitaji kungoja muda mrefu mpaka atakapoweza kuishi maisha yenye kuzaa matunda. Ameitwa na Mungu, ameitwa katika ufalme wake wa Mbinguni, lakini pia ameitwa kwa kazi yake. Si kazi ya mtumwa kwa watu inayofanya maisha yake kuwa yenye thamani bali hali yake ya kuitwa na Mwumba na Mkombozi wake.

Kuenea kwa imani ya Kikristo katika historia imewekwa kuwa jambo la hakika. Mkristo anaweza kumtumikia Mungu kama mtumwa bila mabadiliko yoyote ya hali za nje, na anaweza kujipatia uhuru, na kushughulikia kuachiliwa na kubadili hali hizo. Anayo maisha katika maana timilifu katika kila hali. Kwa sababu tayari ana kila kitu, anaweza kubadilisha kila kitu.

Katika Kol. 3:25-4:1, tunapata maonyo makali kwa mabwana wa watumwa. Wanakumbushwa kuhusu wajibu wao halali kwa sababu Mungu hampendelei mtu. Hata hivyo, mtumwa Mkristo hahitaji kungoja mpaka bwana wake awapo mwenye haki. Anaweza kuishi kwa kulingana na mapenzi ya Mungu hapa na sasa! Si lazima angoje mpaka dunia itakapobadilika kabisa, kama inavyofikiriwa katika Uhindu, Ubudha, Umaksi na dini nyingine!

Kwa mfuasi wa umaksi, kwa hakika mwanadamu na kazi ni vitu pacha. Hawezi kufikiri kazi mbali na mwanadamu, kama anavyomkana pia Mungu awezaye kufanya kazi; na hawezi kumfikiria mwanadamu mbali na kazi ambayo hufanya vitu kama Sabato, muda wa kuburudika au huduma ya Jumapili kuwa mambo yasiyowezekana. Friedrich Engels anaandika:

> "Kazi ni chanzo cha utajiri wote, wachumi wanasiasa hutuambia. Ndio, ni hivyo, mbali na asili ambayo hutupatia vitu ambavyo kazi huvibadili kuwa utajiri. Lakini kazi ni kubwa mno kupita hili. Ni kigezo cha kwanza cha kimsingi cha maisha ya mwandamu na hiki ni kipimo ambacho ni lazima tuseme katika maana yake halisi: Kazi imemwumba mtu mwenyewe."[39]

Kwamba kazi ilimwumba mwanadamu ni njia nyingine ya kusema kwamba mwanadamu alijiumba mwenyewe kama nukuu ifuatayo ya Karl Marx inavyothibitisha:

> "Kwa sababu kwa mtu mshoshalisti chochote kile kiitwacho historia ya dunia si chochote zaidi ya kuwazaa watu kwa njia ya shughuli za mwanadamu, huku ni kuibuka kwa asili kupitia watu, [mshoshalisti] ana

---

[39] Karl Marx. Friedrich Engels. *Werke*. op. cit. Kit. 20. uk. 444

uthibitisho wa wazi na usiopingika wa kuzaliwa kwake kupitia yeye mwenyewe, wa hatua za asili yake mwenyewe."[40]

Kama mwanadamu na kazi ni vitu pacha na kazi ndio thamani kuu ya jamii, kazi hii haitakuwa na thamani chanya iliyothibitishwa na wote, bali itakuwa thamani kandamizi inayochukiwa na wote isipokuwa wachache. Kwa sababu kazi haiko chini ya mamlaka ya Mungu na chini ya uhusika wa mwanadamu, hugeuka kuwa ukandamizaji wenye kutisha. Umaksi hujaribu kupigana na hili bila kutoa kwa uhalisia njia yoyote ya kuepukana nalo. Ikiwa kazi na binadamu ni pacha, inawezekanaje mwanadamu kuepuka ukandamizaji wa kazi pasipo kumpoteza yeye mwenyewe?

Magumu ya kazi

Wakati wote kazi ni kazi kwa ajili ya Mungu. Na mtu hawezi kuzungumza kuhusu kazi bila kuzungumza juu ya Mungu. Hiyo ndiyo sababu kwa nini laana ya dhambi kwa mwanadamu wakati wa Anguko ilikuwa ni laana kwa kazi ya mwanadamu. (Mwa. 3:17-19; 5:29). Mwanadamu alidhani kwamba angeweza kuwa na mamlaka ya utawala na kazi bila yule ambaye huvifanya vyote viwezekane, yaani Mungu. Kwa sababu ya laana, Mwanadamu anakumbushwa mara kwa mara maana ya kumdharau Mwumba. Yeyote atakaye kazi bila matatizo hulikataa Anguko na hukataa kwamba Mungu pekee ndiye awezaye kuwa chanzo cha kazi ambayo huongoza kwenye matokeo kamili na kwenye pumziko la kweli. Kama sio dhabihu ya Nafsi ya pili ya Utatu hakungekuwa na tumaini kwamba hali hii ingebadilika kabisa. Wakati uleule Wakristo wanabeba dhiki na magumu ya kazi kutoka katika mkono wa Mungu. "Je! Mtendakazi anayo faida gani katika yale anayojishugulisha nayo? Nimeona tabu ambayo Mungu amewapa wanadamu, ili kutaabika ndani yake" (Mhu. 3:9-10). Magumu [ya kazi] hutolewa na Mungu. Sulemani hafiki kwenye hitimisho ya kwamba ni vema kutokufanya kazi kabisa bali ni kwamba tunafurahia matokeo ya kazi zetu kama zawadi kutoka kwa Mungu: "Mimi najua kuwa hakuna jema kwao kupita kufurahi, na kufanya mema maadam wanaishi. Tena ni karama ya Mungu kila mtu apate kula na kunywa, na kujiburudisha kwa mema katika kazi yake yote" (Mhu. 3:12-13).

Biblia hutuamuru tuyachukue magumu haya juu yetu sisi wenyewe na si kuweka mzigo juu ya wengine. Ni mwizi pekee ndiye awekaye mzigo juu ya wengine kama ifanyavyo Serikali kwa kutumia kodi kugawa utajiri kutoka mtu mmoja kwenda kwa mwingine. Onyo la upole la Paulo

[40] Rud. Kit. 40. uk. 546

halihitaji kuelezwa kwa kirefu: "Lakini twawasihi, ndugu[41], … Tena mjitahidi kutulia, na kutenda shughuli zenu, na kufanya kazi kwa mikono yenu wenyewe, kama tulivyowaagiza; ili mwenende kwa adabu mbele yao walio nje, wala msiwe na haja ya kitu chochote" (1 Thes. 4:10-12). "Maana twasikia kwamba wako watu kwenu waendao bila utaratibu, hawana shughuli zao wenyewe, lakini wanajishughulisha na mambo ya wengine. Basi twawaagiza hao, na kuwaonya katika Bwana Yesu Kristo, watende kazi kwa utulivu na kula chakula chao wenyewe" (2 Thes. 3:11-12). Kile ambacho Paulo aliwafundisha wengine, yeye pamoja na watendakazi pamoja naye ndicho walichokifanya: "Mwajua wenyewe jinsi iwapasavyo; kwa sababu hatukuenda bila utaratibu kwenu, wala hatukula chakula kwa mtu yeyote bure; bali kwa taabu na masumbufu, usiku na mchana tulitenda kazi, ili tusimlemee mtu wa kwenu awaye yote" (2 Thes. 3:7-8).

Tena Mungu ndiye mfano mzuri zaidi. Alichukua huzuni, magumu na maumivu yote ya kazi ya ukombozi juu yake mwenyewe. Mungu alimtoa Mwanawe wa pekee kutukomboa kutoka kwenye Anguko. Hakuweka mzigo wake juu yetu bali alibeba mizigo yetu juu ya Msalaba. Kama theolojia itampoteza Mungu Mtatu, inampoteza Mungu, ambaye alibeba mizigo ya watu wake wateule. Si Uislamu wala Umaksi, si Ubhudha wala Serikali wenye kitu chochote cha kutoa badala yake.

Kazi ya Mungu ni kazi ya Mgawanyo

3. Kazi ya Mungu Mtatu ni kazi ya mgawanyo. Nafsi za Mungu Mtatu hugawana kazi zao na wote hawana majukumu na kazi ya aina moja, kama *1 Kor 12:4-6* inavyoonesha vizuri. Kwa sababu kazi zao ni tofauti, lakini zikiwa zimeelekezwa kwenye lengo moja, Utatu hudhihirisha jinsi ushirika wa kweli katika upendo na kusaidiana, kwa neno na majadiliano, kwa mpango na ukamilishaji wa mbinu, hata kabla ya Uumbaji. Huu ni *utofauti katika umoja* usioweza kufanya makosa. Ikiwa tu una utofauti katika umoja na umoja katika utofauti, ikiwa tu unaamini katika *Mungu wa Universe* (umoja 'uni-' katika utofauti '-verse'), kazi yaweza kuwa njia ya kutumikiana sisi kwa sisi. Mungu huwataka watu kutumikiana wao kwa

[41] Katika lugha nyingi, wingi wa 'kaka' au wa 'dada' hutumika katika kuwajumuisha pamoja watoto wa kiume na wa kike wa wazazi wamoja. Katika Kijerumani jina la wingi la zamani la 'dada', 'Geschwister' ni jina kwa ajili ya wa-kaka na wa-dada. Mara nyingi katika Kigriki, wingi wa jina hili 'adelphos' (wa-kaka)', 'adelphoi' ('wa-kaka' au 'wa-kaka na wa-dada') hutumika kuwaelezea wa-kaka na wa-dada kwa wakati mmoja. Hakuna neno jingine linalojumuisha maana zote mbili kwa pamoja. (Wingi wa dada 'adelphai' hutumika tu kwa wa-dada.)

wao, kama Nafsi za Utatu zinavyotumikiana kila moja na nyenzake. Tunategemeana kila mmoja na mwenzake kwa sababu tuna miito tofauti, uwezo tofauti, vipawa tofauti, na majukumu tofauti. Msisitizo juu ya vipawa vya Roho kwa Kanisa huthibitisha jambo hili bila mashaka. Mungu hataki kila mmoja afanye sawa na mwingine – isipokuwa tu kwa amri zake – lakini hupenda utofauti wa majukumu, vitendo na matukio katika kanisa na kwingineko.

Familia ni mfano bora kabisa wa kituo cha mgawanyo wa kazi katika maisha. Katika familia watu hujifunza tofauti za jinsia – au hawajifunzi kabisa. Katika familia watu hujifunza kazi tofauti za wazazi na watoto, za wazee na vijana – au hawajifunzi kabisa. Katika familia watu hujifunza jinsi watu tofauti walivyo chini ya Mungu mmoja – au hawajifunzi kukubali kuwa watu wako tofauti. Katika familia, watu hujifunza kwamba maisha na kazi humaanisha kutumikiana kila mtu na mwenzake – au hawajifunzi kabisa.

Ni jambo la kufurahisha kuwa Marx aliona mgawanyo wa kazi kama anguko la mwanadamu lililosababisha matokeo ya haraka ya ndoa na umilikaji binafsi. Mtu aliumbwa kupitia kazi yake, lakini utengano wa mtu na kazi ulitokea kupitia mgawanyo wa kazi. Unyonyaji huja kupitia kazi iliyogawanywa, kupitia ndoa na kupitia umilikaji binafsi. (Hata hivyo: Marx anaongelea juu ya uanzishwaji wa mgawanyo wa kazi, ndoa na umilikaji binafsi kama "Anguko la Kiuchumi" akitumia histilahi ya Kijerumani ('siindenfall') kwa Anguko la mwanadamu lililorekodiwa katika Mwanzo 3. Kwa kutambua anaweka 'anguko' lake katika mahali pa Anguko la kibiblia ambalo lingekuwa uthibitisho wa kutosha kuwa alianzisha uamsho wa dini, na sio nadharia ya kiuchumi. Inahitaji imani kubwa juu ya Anguko la kibiblia kama inavyohitajika kuamini katika Anguko la kimaksi).

Marx alikuwa sawa kuona kuwa hakuna ndoa na hakuna umiliki binafsi bila mgawawanyo wa kazi. Lakini kwa sababu hukiita dhambi kile ambacho Biblia hukitangaza kuwa ni Uumbaji mzuri wa Mungu, hawezi kutoa msaada wowote wa kuushinda unyonyaji. Msaada wake pekee ni unabii wake kwamba siku moja mgawanyo wa kazi utakwisha. Aliandika:

> "Katika hatua ya juu ya Kikomunisti, baada ya utii wa kitumwa wa watu chini ya mgawanyo wa kazi na pamoja nao ukinzani kati ya kazi ya akili na ya mwili kuwa umetoweka; baada ya kazi kutokuwa njia ya kuishi bali yenyewe kuwa kanuni ya kwanza ya maisha, baada ya chemchemi za utajiri wa pamoja kutiririka kikamilifu kupitia maendeleo ya kila mtu binafsi na nguvu zake za uzalishaji; hivyo ndivyo haki ya tabaka jembamba la wenye nacho (bouigeois) yaweza kufungwa na jamii yaweza kuandika kwenye

bango lake: Kila mmoja kwa kadri ya uwezo wake, kila mmoja kwa kadri ya mahitaji yake!”[42]

Marx kamwe haelezei ni jinsi gani jambo hili litawezekana bila ya mgawanyo wa kazi. Kamwe hajibu swali kama mwisho wa mgawanyo wa kazi humaanisha kila mmoja kufanya sawa na mwingine. Kamwe hajibu ni jinsi gani jamii itafanya kazi bila ya mgawanyo wa kazi. Bali alitabiri tu juu ya tumaini lake la umoja kwa sababu alimchukia Mungu Mtatu, aliye chanzo cha utofauti wote.

Kazi ya Mungu ni huduma ya kila mmoja kwa mwingine

Katika Utatu, Nafsi hufanya kazi kila moja kwa nyenzake. Wakati na baada ya Uumbaji, Mungu hufanya kazi kwa ajili ya Uumbaji. Kazi sio tu kazi kwa faida ya yule anayefanya kazi. Kwa wakati uleule, kazi daima ni kwa ajili ya mtu mwenyewe na kwa ajili ya wengine. Ni Mungu Mtatu afanye jambo hilo kuwezekana kwamba kazi ya mtu binafsi na kazi kwa ajili ya wengine havipingani kila moja na nyenzake bali kila wakati huenda pamoja. Kama vile Mungu anavyofanya kazi kwa sababu ya utukufu wake kwa wakati uleule daima hufanya kazi kwa ajili ya Nafsi nyingine ya Utatu na/au kwa ajili ya Uumbaji wake, ndivyo ambavyo kazi ya mwanadamu imebuniwa kumsaidia yeye binafsi na kusaidia wengine.

Kazi ni huduma. Lugha zetu zimechukua dhana hii kutoka kwenye athari ya Kikristo. Tunatumia neno la Kilatini kwa ajili ya mtumishi, ‘mhudumu’, kumwita Mchungaji na vilevile mwanasiasa aliyeko katika cheo cha juu. Inawezekanaje mfanyakazi katika nafasi yenye mamlaka awe ‘mtumishi’? Kwa sababu mamlaka kuu, ambayo ni Yesu Kristo mwenyewe, ni mtumishi. Huwa tunazungumza juu ya ‘mtumishi wa serikali’, juu ya utumishi wa kijeshi, juu ya ‘muda wa utumishi’ na ‘miaka ya utumishi’ badala ya miaka ya kazi.

Kwa hiyo mishahara kamwe haitumiki kwa wafanyakazi pekee.

> “Agano jipya halidunishi ukweli kwamba kazi hutumika kumpatia mtu mahitaji yake ya kuishi (Efe. 4:28; 1 The. 4:11; 2 The. 3:8, 12). Lakini kwa upande mwingine, mishahara haukukusudiwa tu kwa ajili ya yule afanyaye kazi.”[43]

Kiwango maalumu cha mapato, fungu la kumi, ni la Mungu. Jamii na Serikali kihalali wanaweza kuchukua kodi (ijapokuwa kwa kweli si kwa

---

[42] Rud. Kit. 19. uk. 21 (tena katika Kijerumani sentensi hii ni yenye utata zaidi. Hivi ndivyo ilvyo kwa Maksi.)

[43] Hermann Cremer. *Arbeit und Eigentum in christlicher Sicht*. op. cit. uk. 11.

wingi kama siku hizi). Mtu yeyote ambaye halipi kwa ajili ya maisha ya familia yake, ikiwa ni pamoja na wazazi wake, ni mbaya kuliko asiyeamini (1 Tim. 5:8; Mk. 7:9-13). Kuna majukumu mengine ya kijamii.

Mfano mzuri ni maonyo ya Paulo kwa wale waliokuwa wezi hapo kabla: “Mwibaji asiibe tena; bali afadhali afanye juhudi, akitenda kazi iliyo nzuri kwa mikono yake mwenyewe, apate kuwa na kitu cha kumgawia mhitaji” (Efe. 4:28). Tena Paulo hataji kwamba yule aliyekuwa mwizi hapo kabla huishi kwa mapato yake, ingawa hili linaweza kuwa likimaanishwa. Paulo anazungumzia tu uwezekano wa kuwasaidia wengine kama unafanya kazi.

Mungu Akutaka Upende

Upendo ni Utimilifu wa Sheria: Pasipo Sheria Upendo Hufa

Mahubiri ya Mlimani

Tunapoanza kufikiri kuhusu sheria na upendo, kwanza tuchunguze utata kuhusu Mahubiri ya Mlimani. Je, Yesu hapa anatoa amri mpya au anarudia kutamka Sheria ya Agano la Kale? Wale wanaoamini kwamba Yesu anatoa amri mpya katika Mahubiri ya Mlimani, wanaonesha upungufu wa uelewa: 1) wa jibu la Yesu kwa Mafarisayo, 2) wa kifungu chenyewe cha Mahubiri hayo, na hasa 3) wa amri za Agano la Kale.

1) Mara kwa mara, Yesu alitumia Agano la Kale kuwapinga Mafarisayo. Ni kwa namna gani angeweza kutumia Agano la Kale kama mamlaka yake dhidi ya Mafarisayo kama Mafarisayo waliwakilisha Agano la Kale? Mara kwa Mara Yesu aliwakaripia Mafarisayo na waandishi kwa kufasili vibaya, kwa kulitumia vibaya na kwa kulikataa Agano la Kale. Hili linaonekana hasa katika Mk. 7:1-5 (Mat. 15:1-13). Kwa mfano, hapa Yesu anasema: "**Kwa kuziweka kando amri za Mungu, mnashika mapokeo ya wanadamu … Mnayo njia nzuri ya kuweka kando amri za Mungu ili mpate kushika mapokeo yenu wenyewe"** (Mk. 7:8-9). Katika 'Ole' kwa Mafarisayo na waandishi katika Mat. 23 kitambo tu kabla ya unabii wake wa kuharibiwa kwa Yerusalemu katika Mat. 24, Yesu alitangaza: "Ole wenu waandishi na Mafarisayo wanafiki! Kwa kuwa mnalipa zaka za mnanaa na bizari na jira, lakini mmeacha mambo makuu ya sheria, yaani, adili, na rehema, na imani; hayo imewapasa kuyafanya, wala yale mengine msiyaache" (Mat. 23:23).

2) Jambo lile lile linaweza kupatikana katika mahubiri ya Yesu Mlimani. Orodha ya masomo ambayo kila moja huanza na "Mmesikia watu wa kale walivyoambiwa … Bali mimi nawambieni …" (Mat. 5:21-48) hutambulishwa na tamko la wazi kuwa Yesu alikuja kutimiza Sheria. "Msidhani ya kuwa nalikuja kuitangua torati au manabii; la, sikuja kutangua bali kutimiliza" (Mat. 5:17). Alikuja kuimarisha hata "amri moja kati ya hizi zilizo ndogo" (Mat. 5:19, soma Mat. 5:17-20). Je, inawezekana kuwa Yesu alianza orodha hii kwa tamko hili na aliendelea kuzithibitisha sehemu zile za Sheria ambazo angezibatilisha au kuzibadili? Je, hatupaswi kutarajia kuwa Yesu anathibitisha kwa kina kuwa hata ile sheria ndogo

lazima itimizwe? Je, hatutarajii mifano ya haki iliyokosewa iliyofundishwa na Mafarisayo na haki ya kweli ya Yesu?

3) Mifano hii yenyewe inathibitisha kuwa matarajio yetu yako sahihi. Maneno yaliyorudiwarudiwa, 'Lakini mimi nawambieni' katika Mahubiri ya Mlimani moja kwa moja hayako kinyume na Agano la Kale bali dhidi ya theolojia ya Mafarisayo na fasili zao za Agano la Kale. Yesu anaponukuu, "Mmesikia watu wa kale walivyoambiwa …" halinukuu Agano la Kale bali mapokeo na fasili zao za Agano la Kale. Hasemi "Imeandikwa …" kwa sababu kile kilichoandikwa ni sawa na kusema "Lakini mimi nawambieni …".

Yesu anapowaambia wanaomsikiliza "Lakini mimi nawambia, kila mtu atazamaye mwanamke kwa kumtamani, amekwisha kuzini naye moyoni mwake" (Mat. 5:28), haundi dhana mpya ya dhambi ya ndani kinyume na uzoeshi wa nje wa Agano la Kale, bali anawakumbusha wasikilizaji wake kuwa Amri Kumi hazihusu tu amri ya saba dhidi ya uzinzi, bali pia amri ya kumi, "Usimtamani mke wa jirani yako …" (Kut. 20:17; Kumb. 5:21). Vishada vilivyowekwa katika nguo vilikuwa na sababu kuwa, "kuyakumbuka maagizo yote ya BWANA, na kuyafanya; tena kwamba msiende kutanga-tanga kuandama mioyo yenu wenyewe, na macho yenu wenyewe" (Hes. 15:39). Ayubu anasema, "**Nilifanya agano na macho yangu, kutomwangalia msichana kwa tamaa**" (Mith. 31:1). Naye Sulemani atuonya dhidi ya uasherati kwa maneno, "Usiutamani uzuri wake moyoni mwako; wala usikubali akunase kwa kope za macho yake" (Mith. 6:25). Ni katika hali duni kiasi gani ufahamu wa watu wa Agano la Kale ulivyo wakati wasemapo kwamba wazo la dhambi katika kiini cha moyo wa mtu ni wazo jipya! Hata hawajui amri ya kumi ambayo pia huzuia dhambi ya ndani ya tamaa inayoongoza katika wizi (amri ya nane).

Jambo lilelile ni kweli wakati Yesu awakumbushapo Wayahudi kwamba Mungu hazuii tu uuaji halisi bali pia uuaji kupitia mawazo na maneno (Mat. 5:21-26). Katika Agano la Kale, chuki na hasira ni zile dhambi za ndani zinazoongoza katika uuaji wa kidhalimu (mfano, Est. 5:9, Mit. 27:4, Amo. 1:11, Mwa. 49:6-7, Kumb. 19:6, Mit. 16:4). Kama ilivyo kwenye Hotuba Mlimani, Agano la Kale liliruhusu kuua wakati wa kujilinda, wakati wa vita na kwa hukumu ya mahakama ya kisheria tu, lakini sio kwa matakwa ya mtu binafsi. Wajibu wa serikali kuhukumu wahalifu unarudiwa kutajwa na Yesu kwenye Hotuba Mlimani (Mat. 5:25-26; tazama uwiano na Lk. 12:57-59). "Jicho kwa jicho, na jino kwa jino" (Mat. 5:38) haikutolewa kamwe kama amri kwa kisasi binafsi bali kama

moja ya misingi ya hukumu za haki kwenye mahakama za sheria[44] (Kut. 21:23-25; Law 24:19-29; Kumb. 19:21).

Yesu hakatazi watu kuapa, bali anawakataza kuapa kwa kitu chochote kuliko Mungu mwenyewe: "Usiape … kwa mbingu … wala kwa nchi …" n. k. (Mat. 5:34-35; Jak 5:12), kama inavyothibitiswa na kifungu sambamba cha Mat. 23:16-22. Agano la Kale huamuru: "**Mtaapa kwa jina lake**" (Kumb. 6:13; 10:20) na linaendelea kusema: "**Kila aapaye kwa jina lake atamfurahia**" (Zab. 63:11). Kwa hiyo, Paulo anatumia kiapo mara nyingi anapowaandikia Wakristo wapendwa. (2 Kor. 1:23; Flp. 1:8; 1 Thes. 2:5, 10; Rum. 1:9; linganisha na Matendo 21:23 na kuendelea). (Isivyotarajiwa, kwa kulingana na Isa. 65:16 kutakuwa na viapo katika Milenia: "… naye atakayeapa duniani, ataapa kwa Mungu wa kweli"; sawa na Isa. 19:18.)

Ikiwa viapo vilizuiliwa kwa sababu sasa Wakristo wote husema ukweli, tutaelezaje jinsi Mungu aapavyo mwenyewe kwa mamia katika Agano la Kale[45], kwa nini Yesu anaapa mara kwa mara "Amin, Amin" ("kweli, kweli nawaambia") ikiwa ni kanuni moja tu ya viapo alivyotumia. Kulingana na Ebr. 6:19 Mungu aliapa kwa Ibrahimu, "**Kwa sababu alitaka kuweka wazi asili isiyobadilika ya kusudi lake**" (Ebr. 6:19), kwa sababu, "kiapo huthibitisha kile kilichosemwa na kuyafikisha mwisho mabishano" (Ebr. 6:18). Kiapo hakisemi ukweli kwa urahisirahisi tu, huunda kweli ambazo hasiwezi kuvunjwa au kubadilishwa tena. Kiapo huunda agano lenye baraka na laana, jambo ambalo haliwezi kuwa katika kila neno la kweli tulisemalo. Ikiwa kiapo kilikatazwa katika Agano Jipya basi kusingekuwa na uwezekano wa kuoa kwa sababu ndoa ni agano la kiapo. (Mith. 2:16-17; Mal. 2:14; tazama Eze. 16:8; Yer. 5:7).

Nyakati Mpya za Upendo?

Mfano wa mwisho ni muhimu sana kwa somo letu. "Mmesikia kwamba imenenwa, Umpende jirani yako, na, Umchukie adui yako; lakini mimi nawaambini, Wapendeni adui zenu, waombeeni wanaowaudhi …" (Mat.

---

44 Eugen Hühn. *Die alttestamentlichen Citate und Reminiscenzen im Neuen Testament*. J. C. B. Mohr: Tübingen, 1900. kr. 8-9 huonesha kuwa Mafarisayo walitumia sheria hii kimakosa kama jambo lao la kibinafsi na kwamba Yesu hanukuu Agano la Kale moja kwa moja bali fasili ya waandishi kuhusu sentensi hii.

45 Kwa kulingana na Georg Giesen. Die Wurzel sb' "schwören": Eine semasiologische Studie zum Eid im Alten Testament. Bonner Biblische Beiträge 56. Peter Hanstein: Königstein, 1981. uk. 2, neno 'kuapa' (Hebr. sb') pekee limetumika mara 215 katika Agano la Kale, sehemu 75 humtaja Mungu mwenyewe kuwa ndiye mwenye kuapa.

5:43). Je, Yesu anatambulisha nyakati mpya za upendo? La! hasha. Yeyote aliye na ufahamu hata kidogo kuhusu Agano la Kale ni lazima afahamu kwamba amri "Umpende jirani yako, na, Umchukie adui yako" inaenda kinyume na neno na nia ya amri ya Agano la Kale. Inawasilisha mafundisho na utendaji wa baadhi ya Mafarisayo na wandishi, kama vile Otto Michel anavyosema:

> "Hapa Yesu anarejea kwenye aina fulani ya fasili ya Agano la Kale, lakini sio kwenye Agano la Kale lenyewe. Kwa ujumla Yesu anazuia wanafunzi wake kulipa chuki kwa chuki: 'Wapendeni adui zenu, watendeeni mema wale ambao wawachukia ninyi' (Luk. 6:27)"[46].

Kumpenda adui kuna misingi katika Agano la Kale. Ni haki ya Mungu kulipiza kisasi dhidi ya maadui zake. Kwa sehemu amegawa jukumu hili kwa Serikali, ambayo huwaadhibu wahalifu kwa nguvu ya upanga, na kwa Kanisa kupitia upanga wa Roho kwa njia ya kuzitangaza Sheria, kwa kupitia nidhamu ya kanisa na kwa kupitia maombi. Lakini hakuna mtu binafsi ambaye aliruhusiwa kumchukia adui yake binafsi. Mtu hakutakiwa kufurahia anguko la adui yake (Ayu. 31:29). "Adui yako akiwa ana njaa, mpe chakula; tena akiwa ana kiu, mpe maji ya kunywa" (Mith. 25:21)[47]. Sheria inasema kuwa mtu ni lazima amrudishe ng'ombe au punda wa adui wake aliyepotea na, "Ukimwona punda wake huyo akuchukiaye hali ameanguka chini ya mzigo wake" ilimpasa mwamini kumsaidia punda pamoja na maadui zake (Kut. 23:4-5).

Wakati mmoja baba yangu alialikwa kuhutubia kuhusu ikiwa Mungu wa Agano la Kale na Mungu wa Agano Jipya ni mmoja. Alianza kwa kunukuu vifungu kadhaa vya Maandiko akithibitisha kuwa Mungu wa Agano la Kale alikuwa ni Mungu wa upendo na rehema awekaye kando kisasi chake. Halafu akaenda kwenye Kitabu cha Ufunuo akionesha kuwa Mungu wa Agano Jipya ni Mungu wa kisasi ambaye kamwe hatawapenda maadui wake. Basi akawauliza wasikilizaji wake, ni kwa namna gani tunavyoweza kuwianisha Mungu apendaye wa Agano la Kale na Mungu ahukumuye wa Agano Jipya. Mwanzo wasikilizaji wake walichanganyikiwa lakini kwa haraka walilielewa somo.

---

46 Otto Michel. "miseo". kr. 687-698 katika: Gerhard Kittel (mhr.). Theologisches Wörterbuch zum Neuen Testament. Kit. 10. W. Kohlhammer: Stuttgart, 1990 (Toleo lililorudiwa tangu 1933-1979). Kit. IV., uk. 694

47 Sababu ya jambo hili si rehema tu bali pia hukumu ijayo (Mith. 25:22).

"Mpende Jirani Yako Kama Nafsi Yako"

Je, Yesu aliweka upendo mahali pa Sheria? Je, Agano la Kale lililo katili mahali pake palichukuliwa na Agano Jipya lenye amri ya upendo? Hili linawezekanaje ikiwa kiini cha amri ya Agano Jipya "Mpende jirani yako kama nafsi yako" imenukuliwa kutoka katika Agano la Kale?

Hebu na tutazame nukuu hii yenyewe ya Agano la Kale. Katika Law. 19:17 tunasoma: "Usimchukie ndugu yako moyoni mwako; ni lazima kumkemea jirani yako, wala usichukue dhambi kwa ajili yake". Kutokuwa na upande na hali ya kutojali ni vitu vilivyo kinyume na upendo. Ama unamchukia ndugu yako, au utamkemea kwa mujibu Sheria ya Mungu. Ni mstari unaofuata tu usemao: "Mpende jirani yako kama nafsi yako; Mimi ndimi BWANA" (Law. 19:18). Jirani siyo tu jirani wa Kiyahudi bali pia na mgeni: "Mgeni akaaye pamoja nawe atakuwa mzalia kwenu; mpende kama nafsi yako" (Law. 19:34). Mistari hiyo miwili inafunga kifungu kirefu kinachozirudia Amri Kumi na kikizieleza baadhi yake (Law. 19:1-18). Amri kumi hueleza kile Mungu anachomaanisha kwa kumpenda jirani yako, na si tu upendo wa kuishi kwa kulingana na amri hizo, bali pia kuwakemea ndugu wa kiume na wa kike wasioishi kwa kulingana na amri hizo pia. Law. 19:18 inazifupisha amri, hususani Amri Kumi.

Hebu sasa tutazame sehemu nyingi ambako Law. 19:18 imenukuliwa katika Agano Jipya. Hebu tuanze na Yesu mwenyewe. Katika Mat. 19:19 Yesu anafupisha Amri Kumi, ambazo anazinukuu katika toleo fupi kwa kijana tajiri na kiongozi kwa Law. 19:18. Katika Mat. 22:35-40 Yesu anaulizwa na "Mwanasheria" (Mat. 22:36) kutoka katika kundi la Mafarisayo (Mat. 22:35): "Katika torati ni amri ipi iliyo kuu?" (Mat. 22:36). Yesu alijibu kwa kuunganisha Law. 19:18 na Kumb. 6:5: "Mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa akili zako zote. Hii ndiyo amri iliyo kuu, tena ni ya kwanza. Na ya pili yafanana nayo, nayo ni hii, Mpende jirani yako kama nafsi yako. Katika amri hizi mbili hutegemea torati yote na manabii" (Mat. 22:37-40).

Hapa Yesu anaongea kuhusu Agano la Kale. Agano la Kale hutegemea upendo kwa Mungu na upendo wa watu ujao kutoka katika upendo wa kumpenda Mungu. Bila upendo huu, amri zisingekuweko. Katika kifungu chenye kuwiana cha Mk. 12:28-34 Yesu ananukuu amri hizi hizi mbili na kuongeza: "Hakuna amri nyingine iliyo kuu kuliko hizi" (Mat. 12:31). Kwa Waandishi kuuliza swali kunathibitisha kuwa jibu hilo ni sahihi: Kumpenda Mungu na jirani yako "kwafaa kuliko sadaka nzima za kuteketezwa na dhabihu zote pia" (Mat. 12:33). Kwa hiyo Yesu anamwambia "Wewe hu mbali na ufalme wa Mungu" (Mk.12:34). Kila mwandishi angepaswa kujua kwamba amri zote zilikuwa ni kanuni za

upendo tu, na ninataka kusisitiza tena kuwa kile Yesu anachozungumza hapa ni Sheria ya Agano la Kale, siyo jambo jingine jipya.

Kiini cha habari ya Msamaria Mwema pia ni Law. 19:18. Hapa Yesu anamwuliza mwandishi aliyetaka kujua jinsi ya "kurithi uzima wa milele" (Luk. 10:25): "Imeandikwa nini katika torati? Wasomaje?" (Luk. 10:26). Mwandishi anajibu tena kwa kutumia amri ya upendo yenye pande mbili (Luk. 10:27) na Yesu anathibitisha hili kwa maneno: "Fanya hivi nawe utaishi" (Luk. 10:28). Ndipo sasa Yesu anasimulia habari ya Msamaria Mwema, kwa sababu mwandishi alitaka kuomba radhi kwa kutumia fasili yake ya "jirani". Bila kutarajia, baada ya habari ile Yesu haulizi 'Nani aliyekuwa ni jirani?', swali ambalo lingeongoza kwenye jibu 'ni yule aliyeangukia katika mikono ya wanyang'anyi', bali kwa namna kali anauliza: "Waonaje wewe, katika hao watatu, ni yupi aliyekuwa jirani yake …" (Luk. 10:26). Ilimbidi mwandishi akubali kuwa yule mwenye kuonesha huruma ndiye aliyekuwa jirani, na Yesu akamwambia: "Enenda zako, nawe ukafanye vivyo hivyo" (Luk. 10:37).

Kupenda ndiyo amri kuu katika Sheria ya Agano la Kale. Hakuna amri inayoweza kueleweka mbali na upendo. Na upendo hauwezi kueleweka mbali na Sheria.

Paulo alifuata mfano wa Agano la Kale na wa Bwana wake Yesu Kristo. Baada ya kutaja matendo ya mwili (Gal. 5:19-21) anazungumza kuhusu upendo kama tunda la Roho: "Lakini tunda la Roho ni upendo, furaha, amani, uvumilivu, utu wema, fadhili, uaminifu, upole, kiasi" (Gal. 5:22-23). Lakini kwa nini Paulo anaongeza: "juu ya mambo kama hayo hakuna sheria" (Gal. 5:23)? Ni kwa sababu ukionesha upendo, kamwe hutaweza kuvunja amri yoyote. Sheria ni kanuni ya upendo. Kupenda na kutenda jambo kinyume na Sheria ni jambo lenye kujichanganya lenyewe, na haliwezekani kamwe kiufafanuzi. Kwamba hili ndilo jambo ambalo Paulo anataka kulisema huthibitishwa kwa nukuu yake ya Law. 19:18 katika mistari iliyotangulia: "Maana ninyi ndugu[48], mliitwa mpate uhuru; lakini uhuru wenu usiwe sababu ya kuufuata mwili, bali tumikianeni kwa upendo. Maana torati yote imetimilika katika neno moja, nalo ni hili, 'Umpende jirani yako kama nafsi yako'" (Gal. 5:13-14). Uhuru wa Mkristo

[48] Katika lugha nyingi, wingi wa 'kaka' au wa 'dada' hutumika katika kuwajumuisha pamoja watoto wa kiume na wa kike wa wazazi wamoja. Katika Kijerumani jina la wingi la zamani la 'dada', 'Geschwister' ni jina kwa ajili ya wa-kaka na wa-dada. Mara nyingi katika Kigriki, wingi wa jina hili 'adelphos' (wa-kaka)', 'adelphoi' ('wa-kaka' au 'wa-kaka na wa-dada') hutumika kuwaelezea wa-kaka na wa-dada kwa wakati mmoja. Hakuna neno jingine linalojumuisha maana zote mbili kwa pamoja. (Wingi wa dada 'adelphai' hutumika tu kwa wa-dada.)

si uhuru wa kuvunja Sheria bali ni uhuru wa kupenda na wa kuonesha upendo katika mtindo wa kushangaza.

Tamko la wazi la ujumbe huu linaweza kupatikana katika Rum. 13:8-10: "Msiwiwe na mtu chochote, isipokuwa kupendana; kwa maana ampendaye mwenzake ameitimiza sheria. Maana kule kusema, Usizini, Usiue, Usiibe, Usitamani; na ikiwapo amri nyingine yoyote, inajumlishwa katika neno hili, ya kwamba, Mpende jirani yako kama nafsi yako. Pendo halimfanyii jirani neno baya; basi pendo ndilo utimilifu wa sheria." Paulo ananukuu Amri Kumi kwa kifupi, lakini anaongeza kwamba anazungumzia kuhusu "kila amri".

Kila amri inatawaliwa na upendo, inatoka kwenye kiini cha upendo na husema tu kile ambacho upendo hufanya. Yule apendaye kikwelikweli, kamwe hataiba, hataua, hatatamani au hatafanya uzinzi! Ikiwa Wakristo hawatarudi kwenye mantiki hii na motisha ya Amri Kumi na Sheria yote, basi wataomba radhi kwa Sheria ya Mungu kwa sababu wao wenyewe hawajui kwa nini wanashika mambo yake yote.

Wanafikra wa Uyumanisti wa Kimagharibi wameshachukua kiini cha upendo kutoka katika Ukristo, lakini wanachukua tu neno lenyewe kwa sababu wanataka kuamua wenyewe ni kipi upendo huamuru, na upendo ni kitu gani. *Wanataka uhuru mbali na sheria, si uhuru* ***katika*** *sheria na hivyo kutengeneza* ***upendo mbali na sheria,*** *sio* ***upendo kulingana na sheria***. Mara ya mwisho tunaona Law. 19:18 inanukuliwa katika Waraka wa Yakobo. Kwa urahisi Yakobo anaimarisha mahusiano haya baina ya uhuru na Sheria.[49] Yakobo anawakemea wasomaji wake kwa sababu waliwapendelea matajiri, na kuwabagua na kunyanyasa maskini (Yak. 2:1-8). Anathibitishaje jambo hili la kikanisa, kijamii na kiuchumi? Anaandika: "Lakini mkiitimiza ile sheria ya kifalme kama ilivyondikwa, Mpende jirani yako kama nafsi yako, mwatenda vema. Bali mkiwapendelea watu, mwafanya dhambi na kuhukumiwa na sheria kuwa wakosaji. Maana mtu awaye yote atakayeishika sheria yote, ila akajikwaa katika neno moja, amekosa juu ya yote. Kwa maana yeye aliyesema, Usizini, pia alisema, Usiue. Basi ijapokuwa hukuzini, lakini umeua, umekuwa mvunja sheria. Semeni ninyi, na kutenda kama watu watakaohukumiwa kwa sheria ya uhuru" (Yak. 2:8-12).

---

[49] Yakobo hapa anawandikia Wakristo wa Agano Jipya! Je, kuna mtu yeyote awezaye kuelezea ni kwa namna gani mafundisho kwamba Sheria ya Agano la Kale si sheria ya maadili ya Wakristo tena yangeweza kuibuka katika mtazamo wa tamko kama hili? Luther alikuwa na msimamo wa kuuweka pembeni waraka wa Yakobo ili kudumisha mtazamo wake kuwa Agano la Kale ni duni kuliko Agano Jipya.

Sheria, na hasa Amri Kumi, kwa mara nyingine imefupishwa katika Law. 19:18. Amri ya kupenda inaitwa "Sheria ya kifalme". Sheria ya kifalme ni sheria inayotawala amri nyingine zote. Sheria hii ya kifalme pia inaitwa "Sheria ya uhuru". Upendo wa Mungu, Sheria ya Mungu na uhuru wa Mungu vyote ni kitu kile kile. Ama uwe na vyote vitatu au uwe huna hata kimoja. Hakuna upendo bila uhuru, hakuna sheria bila upendo, hakuna upendo bila Sheria na hakuna uhuru bila Sheria.

Upendo ni nini?

Wilhelm Lütgert ameandika katika kitabu chake kiitwacho "Maadili ya Upendo":

> "Amri ya kupenda humaanisha kuwa upendo ni jukumu. Upendo unaagizwa na ni utiifu. Jambo hili linapingwa – upingwaji huu hasa ulifanywa na [mwanafalsafa wa Kijerumani aitwaye Immanuel Kant] – kwamba unaweza tu kuamrisha matendo ya nje (yanayoonekana), lakini si upendo."[50]

Kant alisema kwamba upendo ni uamuzi wa dhamiri huru na wa ndani sana, tena ni hisia ambazo hatuwezi kuzidhibiti. Lütgert anakataa dhana hii lakini anakubali kwamba upendo ni jambo tusiloweza kulizalisha:

> "Kwa hiyo, upendo unaweza kuagizwa na yule aliye na uwezo wa kuuamsha huu upendo. Kwanza upendo ni kitu kinachotolewa kabla hakijawa kitu cha kuagizwa. Upendo ni kipawa kabla haujawa jukumu. Unatolewa kabla haujaamriwa. Unaweza tu kuwa na asili yake katika upendo, na kila wakati ni upendo unaorudishwa. Kwa sababu hii unaweza tu kuwa upendo kutoka kwa Mwumbaji, mwangwi wa pendo lake. Na kwa kuwa ni upendo wa Mwumba mwenyewe, upendo huu utakuwa na uwezo wa uumbaji. Kuhusiana na upendo, kanuni ya Augustine ni halali: 'Toa kile unachoamrisha halafu amrisha kile unachotaka'[51]."

Tunahitaji kufafanua asili ya upendo ili kuweza kuelewa uhusiano kati ya upendo na Sheria.

1) Upendo ni wajibu, kwa sababu tuna "wajibu [au deni] kupendana sisi kwa sisi" (Rum. 13:8; 1 Yoh. 4:11).

2) Upendo ni utii. Kulingana na 1 Pet. 1:22 tunaji "takasa" nafsi zetu kupitia "utii" "kuufikilia upendano wa ndugu"[52]. Hata Yesu alionesha

---

50 Wilhelm Lütgert. *Ethik der Liebe*. Beiträge zur Förderung christlicher Theologie. Reihe 2, Kit. 29. C. Bertelsmann: Gütersloh, 1938. uk. 30

51 Rud.

52 Tazama rejea hapo juu kuhusu 'wa-kaka na wa-dada'.

upendo wake kwa Baba kwa kumtii **"… kama vile mimi nilivyozitii amri za Baba yangu na kukaa katika pendo lake**" (Yoh. 15:10).

3) Upendo ni kitendo cha moyo na dhamiri. Tunaambiwa tuwe na "**nia moja na … upendo**" (Flp. 2:2), ambao "nia hiyo hiyo … ambayo imo pia ndani ya Kristo" (Flp. 2:5).

4) Upendo ni halisi, ni kitu cha kweli, kilichopo na cha vitendo, na ni tendo. 1 Yohana 3:17-18 yasema: "**Ikiwa mtu ana mali za dunia hii, kisha amwona ndugu yake ni mhitaji, lakini anamzuilia huruma zake, yawezekanaje upendo wa Mungu kuwa ndani yake? Watoto wapendwa, tusipende kwa maneno au kwa ulimi, bali kwa vitendo na katika kweli**". Yohana anaimarisha hili kwa kielelezo cha Yesu. Upendo wa Yesu hauthibitishwi kwa hisia za ndani, maneno mazuri au mipango mikubwa, bali kwa kielelezo alichokifanya kwa ajili yetu. "Katika hili tumelifahamu pendo [la Mungu], **Yesu Kristo aliutoa uhai wake kwa ajili yetu**" (1 Yoh. 3:16; ni sawa na Rum. 5:8; Yoh. 3:16; Efe. 5:25). Katika Waefeso 5:25-33 mume anathibitisha pendo lake kwa mkewe kama Kristo anavyothibitisha pendo lake kwa Kanisa kwa kuwa tayari kufa kwa ajili yake na kwa kumlisha na kumtunza. Paulo anatuambia kwamba "katika Kristo Yesu", "nguvu" pekee "ni imani itendayo kazi kwa upendo" (Gal. 5:6). Katika Ufunuo 2:4-5 Kanisa la Efeso linaamriwa kurudia "upendo wa kwanza" ambao liliuacha: "ukatubu, ukayafanye matendo ya kwanza". Katika Ufunuo 2:19 Yesu anajua "matendo yako na upendo na imani … yako".

Kumpenda Mungu ni kutii Sheria Yake

Sasa tunaelewa vyema sababu inayofanya upendo uwe utimilifu wa sheria. Mara nyingi, Biblia husema kuwa maana kamilifu ya Sheria ni kufafanua na kuuendeleza upendo. Paulo anamwandikia Timotheo: "**Lengo [Kigriki: 'telos'] la amri hiyo ni upendo utokao katika moyo safi na dhamiri njema, na imani isiyo na unafiki**" (1 Tim. 1:5).

Kumcha, kumtumikia na kumpenda Mungu na kupenda Sheria yake na amri zake kila wakati kunalinganishwa katika Agano la Kale na katika Agano Jipya. **"Mpende BWANA Mungu wako na ushike matakwa yake, amri zake, sheria zake na maagizo yake daima"** (Kumb. 11:1). **"Ikiwa utatunza kwa makini maagizo haya yote, nimekupa kumfuata, kumpenda BWANA Mungu wako, kutembea katika njia zake zote na kushikamana naye …"** (Kumb. 11:22). **"… Kwa sababu unafuata kwa makini sheria hizi zote nilizokuamuru leo, kumpenda BWANA Mungu wako na kutembea daima katika njia zake …"** (Kumb. 19:9).

Katika Amri Kumi, Mungu hutuahidi kutupatia "neema" na baraka kwa "wote wanipendao, na kuzishika amri zangu" (Kut. 20:6; Kumb. 5:10).

Dan. 9:4 na Neh. 1:5 huzungumza kuhusu "Mungu ashikaye agano lake la upendo kwao wampendao, na kuzishika amri zake" (ni sawa na Kumb. 7:9). Katika 1 Wafalme 3:3 imeandikwa: "Sulemani naye akampenda BWANA akienda katika amri za Daudi babaye".

Je, hii ndio lugha na nia pekee ya Agano la Kale? La, hasha. Hebu sikiliza maneno sawa na hayo kupitia kwa kinywa cha mtoa sheria mwenyewe Yesu Kristo: "Mkinipenda, mtazishika amri zangu" (Yoh. 14:15). "Yeye aliye na amri zangu, na kuzishika, yeye ndiye anipendaye; naye anipendaye atapendwa na Baba yangu …" (Yoh. 14:21). **"… Mtu akinipenda, atayashika mafundisho yangu … Mtu asiyenipenda, hatayashika mafundisho yangu …**" (Yoh. 14:23-24). "Kama vile Baba alivyonipenda mimi, nami nilivyowapenda ninyi, kaeni katika pendo langu. Mkizishika amri zangu, mtakaa katika pendo langu; kama vile mimi nilivyozishika amri za Baba yangu na kukaa katika pendo lake … Amri yangu ndiyo hii, Mpendane, kama nilivyowapenda ninyi." (Yoh. 15:9-10, 12).

Yohana, aliyenakiri haya yote, aliandika kwenye waraka wake mwenyewe kwamba: "**Hivi ndivyo tujuavyo kuwa twawapenda watoto wa Mungu, kwa kumpenda Mungu na kutekeleza amri zake. Upendo wa Mungu ni huu: kuzitii amri zake. Na amri zake si nzito**" (1 Yoh. 5:2-3). "**Twajua kuwa tumepata kumfahamu yeye ikiwa twazitii amri zake. Mtu asemaye: Namjua na hatendi Mungu anachokiamuru, ni mwongo, na ukweli haumo ndani yake. Ikiwa yeyote hutii maneno yake, kwa hakika upendo wa Mungu unafanywa kuwa kamili ndani yake**" (1 Yoh. 2:3-5). "**Na hii ndio amri yake, kuamini katika jina la mwana wake Yesu Kristo, na kupendana sisi kwa sisi kama alivyotuamuru. Wale wanaozitii amri zake huishi ndani yake na yeye ndani yao**" (1 Yoh. 3:23).

Je, hii inamaanisha kuwa ni lazima tuufanyie kazi wokovu wetu? La, hasha! Ikiwa Sheria ya upendo, upendo kwa Mungu na upendo wa Mungu ni kitu moja, basi huwezi kupenda bila Mungu. Ikiwa tungepaswa kumpenda Mungu kwanza kabla ya Mungu kutupenda, upendo usingewezekana. "Bali Mungu aonyesha pendo lake yeye mwenyewe kwetu sisi, kwa kuwa Kristo alikufa kwa ajili yetu, tulipokuwa tungali wenye dhambi" (Rum. 5:8). Lakini kama unapendwa na umechaguliwa na Mungu, upendo huu kamwe huwezi kuuishi na kuuelewa mbali na Sheria.

"Mungu ni upendo" (1 Yoh. 4:8, 16). Yeye ni "Mungu wa upendo" (2 Kor. 13:11) na Yesu ndiye "**upendo wa Mungu kati yetu**" (1 Yoh. 4:9). Kwa hiyo upendo unaweza kuwa na asili yake katika Mungu tu, kama Yohana asemavyo "pendo latoka kwa Mungu" (1 Yoh. 4:7). Kwa hiyo ni jambo lile lile kuwa katika Mungu na kuwa katika upendo wake: "Mungu

ni upendo, naye akaaye katika pendo, hukaa ndani ya Mungu, na Mungu ukaa ndani yake" (1 Yoh. 4:16). Vivyo hivyo, kumjua Mungu na kumpenda ni sawa. "… na kila apendaye amezaliwa na Mungu, naye anamjua Mungu. Yeye asiyependa hakumjua Mungu, kwa maana Mungu ni upendo" (1 Yoh. 4:7-8). Mungu aliposema kupitia kwa Hosea kuwa "**kwa sababu hapana kweli, wala upendo, wala kumjua Mungu katika nchi.**" (Hos. 4:1), hazungumzii matatizo kadha wa kadha bali ni kuhusu jambo moja tu, upendo.

Injili na Sheria

Mjadala wote usio na matunda kuhusu Injili na Sheria umeficha ujumbe wa Biblia kwamba Sheria ni udhihirisho wa upendo wa Mungu. Hakuna Injili bila upendo. Lakini ikiwa upendo unadhihirishwa na kuratibiwa na Sheria ya Mungu, basi hakuwezi kuwa na Injili bila Sheria. Tuangalie mifano miwili tu ambapo Paulo anazungumza kuhusu 'sheria' na 'injili' katika kifungu kili kile:

Katika 1 Tim. 1:9-11 Paulo hungumzia kuhusu matumizi mabaya na matumizi ya kitauwa ya Sheria. Kisha anataja mifano ya wavunja sheria kama 'wauaji' au 'wafanya biashara ya watumwa', wanaohukumiwa na Sheria, na anaendelea kusema: "… na likiwepo neno lolote linginelo lisilopatana na mafundisho yenye uzima; kama vile ilivyonenwa katika Habari njema ya utukufu wa Mungu" (1 Tim. 1:11). Katika Rum. 2:12-15, Paulo anaeleza hukumu ya Wayaudi na ya watu wa mataifa kupitia Sheria na anafunga mjadala huu kwa maneno: "**Hii itatokea katika siku ambayo Mungu atahukumu siri za wanadamu katika Yesu Kristo, kwa mujibu wa Injili yangu**" (Rum. 2:16). Je, una kifaa cha kutenganisha Injili na Sheria katika vifungu hivi? Sheria ya Mungu ni Injili kwa watoto wake na Injili yake ni hatari kuu kwa maadui zake.

Injili na Sheria husimama kinyume cha kila moja na nyenzake – hasa katika nyaraka za Paulo – ikiwa sheria itaeleweka kama wokovu kwa njia ya Sheria, lakini si kama Sheria itaeleweka kama Sheria ya Mungu iliyoandikwa katika Agano la Kale na Agano Jipya.

Pasipo Sheria Upendo Hufa

Upendo na sheria viko pamoja. Kwa hiyo, ukosefu wa sheria huongoza katika ukosefu wa upendo[53] (ukosefu wa wema). Upendo ni utimilifu wa

[53] Kijerumani hutumia neno 'Lieblosigkeit', 'kukosa upendo', neno hili huundwa sawa na 'Gesetzlosigkeit', 'kukosa sheria'. Kwa hivyo tumia neno ukosa upendo, kwa kuwa 'ukosa wema' ni kudhaifisha somo langu.

Sheria na pasipo Sheria, upendo hufa. Jambo hili ni kweli kwa maagano yote yaliyotolewa na Mungu. Bila Sheria hakungekuwa na upendo katika ndoa na katika familia. Bila Sheria hakungekuwa na upendo kanisani. Bila sheria hakungekuwa na upendo katika mahusiano na shughuli za kikazi. Bila sheria hakungekuwa na upendo katika jamii. Bila sheria hakungekuwa na upendo katika serikali za mtaa na serikali kuu. Hakuna kifungu katika Agano la Kale na katika Agano Jipya kinachoeleza haya moja kwa moja kuliko unabii wa Yesu katika Mat. 24:12 "**na kwa sababu ukosefu wa sheria utakuwa mwingi, upendo wa wengi utapoa**"[54].

Ninafikiri hakuna kifungu katika Biblia kinachofafanua waziwazi zaidi, kwa kifupi na moja kwa moja tatizo la Uyumanisti wa wakati wa sasa na vile vile mtazamo wa Kiinjili wa wakati wa sasa kuliko hiki: "**na kwa sababu ukosefu wa sheria utakuwa mwingi, upendo wa wengi utapoa**". Ni katika kuurudia upendo wa Mungu na Sheria zake tu ndipo tutaweza kurudisha upendo katika familia zetu, makanisa yetu, mahusiano yetu ya kikazi, ya kijamii na kiserikali. Ni katika kuurudia upendo wa Mungu na Sheria zake tu ndipo tunaweza kuelekea katika ujenzi mpya wa kila eneo la maisha yetu. Kwa hiyo, tumpende Mungu zaidi na zaidi na tuishi katika Sheria zake na tuitangaze kwa kanisa lisilo na sheria na lisilo na upendo na kwa jamii isiyo na sheria na isiyo na upendo.

Ikiwa upendo ni kichocheo na lengo la Sheria, hatutampenda tu mwanzilishi wa Sheria yaani Mungu Baba, Mungu Mwana na Roho Mtakatifu, bali pia tutaipenda sheria yake yenyewe kama tuonavyo mara kadha wa kadha katika Zaburi. "***Ninayo nia kuyafanya mapenzi yako, Ee Mungu wangu, Sheria yako iko ndani ya moyo wangu***" (Zab. 40:8 – Paulo anatumia kifungu hiki katika Rum. 7:22). "***Ni jinsi gani niipendavyo Sheria yako! Ninatafakari juu yake mchana kutwa***" (Zab. 119:97; tazama Zab. 119:47-48, 113, 119, 127-128, 159, 163, 165, 167). Baada ya Daudi kuimba juu ya Uumbaji na Mwumbaji wake katika Zaburi 19, anaendelea na wimbo wa Sheria, ambao ninamaliza nao hapa:

> "Sheria ya BWANA ni kamilifu, huiburudisha nafsi. Ushuhuda wa BWANA ni amini, humtia mjinga hekima. Maagizo ya BWANA ni ya adili, huufurahisha moyo. Amri ya BWANA ni safi, huyatia macho nuru. Kicho cha BWANA ni kitakatifu, kinadumu milele. Hukumu za BWANA ni kweli, zina haki kabisa. Ni za kutamanika kuliko dhahabu, kuliko wingi wa dhahabu safi. Nazo ni tamu kuliko asali, kuliko sega la asali. Tena mtumishi

---

[54] Nilitumia toleo la King James lakini nikabadilisha "uovu" kuwa "ukosa sheria", hii ni tafsiri nzuri zaidi ya neno la Kigriki 'anomia', "kukosa sheria". Vifungu vingine vyote vya Biblia vimetafsiriwa na mwandishi kutoka katika toleo la Kigriki.

wako huonywa kwazo, katika kuzishika kuna thawabu nyingi. Ni nani awezaye kuyatambua makosa yake? Unitakase na mambo ya siri. **Umzuie mtumishi wako asitende dhambi za kiburi, zisinitawale mimi. Ndipo nitakapokuwa kamili, nami nitakuwa mwenye haki mbali na kosa lililo kubwa . Maneno ya kinywa changu, na mawazo ya moyo wangu, yapate kibali mbele zako, Ee BWANA, nguvu zangu, na mkombozi wangu"** (Zab.19:7-14, Union Version; iliyokolezwa KJV).

Mungu Akutaka Usaidie

Jukumu la Kijamii katika Kanisa la Agano Jipya Kulingana na Matendo ya Mitume 6

Kuchaguliwa kwa mashemasi katika Matendo ya Mitume 6 na katika kanisa la Agano Jipya kwa ujumla ni jambo lenye umuhimu mkubwa. Inashangaza, kwamba mbali na ofisi za waangalizi (maaskofu) na wazee, ambao waliwajibika kwa masuala ya uongozi na kufundisha; kanisa lilikuwa na ofisi nyingine moja tu, ambayo ni ya wahudumu wa kiume na wahudumu wa kike, ambayo kazi yake ilikuwa ya mambo ya kijamii kabisa. Jukumu la kijamii la kanisa kwa washirika wake limetaasisiwa katika ofisi ya wahudumu (mashemasi), kiasi kwamba kanisa bila wao ni jambo lisilofikirika sawa na kanisa pasipo uongozi au mafundisho ya Biblia.

1) Kanisa hujitwika kikamilifu wajibu wa kijamii wa washiriki wake, endapo familia ya mtu mwenyewe haiwezi kufanya hivyo. Kazi hii hujumuisha zaidi ya utoaji wa misaada au usaidizi kwa wachache, bali ni katika kuwajibika kwa wote.

2) Kwa hiyo kanisa ni lazima litofautishe kwa uwazi kati ya majukumu yake ya kijamii kwa wapendwa Wakristo na wajibu wake wa kijamii kwa wengine. Jukumu la kwanza limetaasisiwa katika ofisi ya wahudumu na linabaki hivyo daima, endapo kuna upatikanaji wa fedha na uwezekano (tukichukulia kwamba mtu huyo hakujiletea hali hiyo kwa mapenzi yake mwenyewe). Mithali 3:27 huzungumza hali zote mbili, “Usiwanyime watu mema yaliyo haki yao, ikiwa katika uwezo wa mkono wako kuyatenda.” Wagalatia 6:10 huzungumzia wajibu wetu kwa kila mtu, hata hivyo husisitiza kipaumbele kipewe waamini: “Kwa hiyo kadiri tupatavyo nafasi na tuwatendee watu wote mema; na hasa jamaa ya waaminiyo.”

Amri katika Mat. 24:45 yapaswa pia ieleweke kwa maana hii. Yesu anazungumza kuhusu waamini, si kumhusu kila mtu. Endapo neno “ndugu” lililotajwa katika mstari wa 40 lilikusudiwa kumaanisha watu wote, basi hiki kingekuwa kifungu pekee katika Agano Jipya ambacho kimetumia neno hilo kimafumbo kumwelezea mtu yeyote mbali na washiriki wa kanisa au Wakristo wenzetu.[55]

---

[55] Kurt Hennig, “Beim Wort kommt es auch auf die Worte an”, Das Fundament, (DCTB) 1, l991, kr. 9-24 (hususani kr. 22 na 19-24)

Mlinganisho wa [suala hili] na suala la ufanyaji wa amani (upatanishi) utasaidia kulifafanua jambo hili. Maandiko huwaamuru Wakristo kuishi kwa amani na waumini wenzao. Kama hawafanyi hivyo, uongozi wa kanisa hauna budi kuingilia kati. Kwa namna uhusiano na wale wasio Wakristo ulivyo, Paulo asema, "Kama yamkini, kwa upande wenu, mkae katika amani na watu wote" (Rum. 12:18). Kanisa la Agano Jipya limejengwa juu ya agano ambalo humfunga kila mwamini. Matarajio ya kuwa mwamini anatakiwa kuwajali watu wote huchipukia kutoka katika mtazamo potovu wa uungwana na haki, kwa kuwa Biblia humhitaji mwamini kwanza kuipatia mahitaji familia yake mwenyewe, kisha kwa washiriki wa kanisa lake, hatimaye kwa kanisa ulimwengu mwote. Ni baada tu ya majukumu haya kutimizwa, ndipo anapokuwa na wajibu kwa watu wengine.

3) Matendo 6 hutoa kipaumbele kikubwa kwa jukumu la kijamii la kanisa kwa washiriki wake, lakini wajibu wa kutangaza Neno la Mungu na maombi hubaki kuwa wenye umuhimu zaidi na umetaasisiwa katika ofisi ya wazee na mitume.

Mitume wanatoa sababu ifuatayo ya kukataa kulikubali "jambo" hili (Matendo 6:3), "na sisi tutadumu katika kuomba na kulihudumia lile Neno" (Matendo 6:4). Maombi na utangazaji wa Neno, vitu ambavyo daima huwa viko pamoja, vina kipaumbele kuliko kujihusisha na masuala ya kijamii na ni mambo yasiyopaswa kutelekezwa. Mwunganiko wa maombi na mafundisho si jambo geni. Muda mrefu huko nyuma, ilikuwa ni huduma ya nabii Samweli na viongozi wengine wa Agano la Kale "kuomba" na "kufundisha" (1Sam. 12:23).[56]

Utoaji msaada kwa wasiojiweza kijamii pia lilichukuliwa kuwa ni suala muhimu katika Kanisa la Mwanzo, ambalo mahali pote liliweka mifuko maalumu kwa ajili ya malengo ya kijamii[57]. Usaidizi wake kwa wajane ulikuwa ni kielelezo[58]. Ni jambo la kweli kuwa fedha nyingi zilitumika kwenye shughuli za kijamii kuliko kwenye mishahara ya wazee na wachungaji. Kwa mujibu wa Baba wa Kanisa aitwaye Eusebius, kwa mfano, kanisa la Rumi katika mwaka 250 B.K. liliwasaidia wachungaji 100 na watu 1500 maskini hususani wajane na mayatima. Alois Kehl anaandika:

---

[56] Linganisha mwunganiko wa maombi na kukesha katika Neh. 4:9.

[57] Adolf von Harnack, *Die Mission und Ausbreitung des Christentums in den ersten drei Jahrhunderten* (VMA-Verlag: Wiesbaden, o. J., toleo lililorudiwa mwaka 1924[4]), kr. 178-183, na sura, "Das Evangelium der Liebe und Hilfsleistung", kr. 170-220

[58] Rud. kr. 184-186

> "Kamwe, katika wakati wote wa hapo kale, hakujawahi kuwapo jamii au kikundi cha kidini ambacho kiliwahudumia washiriki wake kama Kanisa la Kikristo lilivyofanya."[59]

Hata hivyo, zaidi ya yote, wajibu wa matajiri, wa kuwasaidia maskini, hauwapi wafadhili haki maalumu kanisani. Kwa sababu hii, Yakobo 2:1-13 anashambulia kwa nguvu majaribio yao ya kutumia nafasi zao vibaya katika kanisa.

---

[59] Rud. kr. 182-184

Mungu Akutaka Uende

Sababu za Kibiblia Kuhusu Umisheni wa Kiinjili: Hoja 31[60]

Dokezo 1. Hoja zifuatazo hazinuii kuwasilisha msimamo wa kitheolojia wa mwandishi mwenyewe, bali kuunda uhalalisho wa kibiblia wa mafundisho yaliyozoeleka kwa wengi wa wamishenari wa kiinjili. Mwandishi anafahamu kuwa ujumuishi huu kamwe hauwezi kuakisi mitazamo yote kwa utoshelevu, na kwamba maoni yake binafsi daima yataonyeshwa waziwazi. Kwa sababu hii, amechagua jina "Sababu za Kibiblia" badala ya "Sababu Maalumu za Kibiblia", kama kwamba anawasilisha mafundisho ya umisheni wa Kiinjili kwa ujumla.

Dokezo 2. Hoja zifuatazo hazinuii kuwasilisha muhtasari wa mafundisho ya Kikristo. Zinakubali Imani ya Mitume, na mafundisho makuu ya kidogma ya Kanisa la Kwanza (Utatu, Yesu mwanadamu kamili na Mungu kamili) na ya Soteriolojia ya Matengenezo (Wokovu kwa Imani, na Maandiko kama mamlaka kwa ajili ya imani na wokovu), n.k.

Sehemu 1: Umisheni wa Kiulimwengu ni sehemu muhimu ya Ukristo

Hoja 1: Mungu alikuwa mmishenari wa kwanza.

Mungu alikuwa, na ni mmisheni wa kwanza. Baada ya Anguko la Mwanadamu, historia ya mwanadamu ilionekana inafikia kikomo. Hata hivyo, Mungu hakuachilia mambo yabaki kama yalivyokuwa, bali alikuja yeye mwenyewe, katika neema na rehema yake, kwenye Bustani ya Edeni kuwatafuta Adamu na Hawa (Mwa. 3:8-9). Aliwatangazia wote Hukumu na Wokovu utakaokuja (Mwa.3:14-21).

---

60 Hoja hizi ziliwasilishwa kama mfumo wa kawaida wa umisheni wa kiinjili katika jubilei ya kumi ya jarida la "Evangelikale Missiologie" linalomilikiwa na "Association of German evangelical missiologists" (AfeM) mnamo mwaka 1994 na kuchapishwa na toleo la jubilei la jarida hili na vilevile kuchapwa na majarida mengine ya kiinjili katika ulimwengu unaozungumza Kijerumani na huko Uholanzi. Toleo hili ni toleo lililoboreshwa, na kufanya matamko kuwa 31 badala ya yale 30 ya kwanza.

Hoja 2: Yesu ndiye kielelezo halisi cha umishenari.

Mungu Baba alimtuma Yesu duniani kama mwanadamu ili aibebe adhabu msalabani, na kuuleta na kuutangaza wokovu. Kabla ya Uumbaji (Efe. 1:4), Mungu alikuwa amekwishaamua tayari kuwa hatamwachilia mwanadamu agubikwe na maangamizi yake mwenyewe, bali kujituma yeye mwenyewe ulimwenguni kama mmishenari katika Yesu (Yoh 3:16).

Hoja 3: Huduma ya kanisa la Kristo imekitwa katika kule kujituma kwa Mungu mwenyewe ulimwenguni kama mmishenari (Missio Dei).

Agano Jipya huona utumwaji wa wanafunzi (mitume) kama mwendelezo wa moja kwa moja wa Mungu kumtuma Kristo (Mat. 10:40; Mk. 9:37; Luk. 10:16; Mdo. 3:20, 26; takribani zaidi ya mara 50 [hamsini] katika Injili ya Yohana; kwanza katika Yoh. 3:17. Tazama Isa. 48:16) na wa Baba na Mwana kumtuma Roho Mtakatifu (Yoh. 14:26; 15:26; Luk. 24:49). Katika Yoh. 17:18, Yesu anasema, “Kama vile ulivyonituma mimi ulimwenguni, nami vivyo hivyo naliwatuma hao ulimwenguni.” Katika Yohana 20:21, anazungumza na wanafunzi wake, “… kama Baba alivyonituma mimi, mimi nami nawapeleka ninyi.” Mungu Baba anawatuma Mwanawe na Roho wake kama wamishenari wa kwanza. Kanisa huliendeleza jukumu hili kupitia umisheni wa kiulimwengu. Kanisa la Agano Jipya lipo kwa kusudi hili. Umisheni wa Kikristo umekitwa katika Mungu Mtatu na katika kujituma kwake mwenyewe.

Hoja 4: Yesu aliwachagua Kumi na Wawili tu kwa kusudi la kuwaandaa kwa ajili ya kutumwa kwao ulimwenguni.

Yesu aliwachagua wanafunzi “wapate kuwa naye, na kwamba awatume kuhubiri” (Mk. 3:13). Tangu mwanzo, lengo la mafunzo yao ya kina kupitia maisha na kufanya kazi pamoja naye lilikuwa ni kuwaandaa kwa Agizo Kuu. Mafunzo yao kama wamishenari hayakuwa ya bahati, bali yalikuwa kwa mujibu wa mpango wake wa kimakusudi. Kwa mfano, fuatilia hatua zifuatazo. 1) Kwanza, Yesu alihubiri peke yake; 2) kisha akahubiri wakati wanafunzi wakitazama. 3) baadaye, akawaacha wanafunzi wahubiri huku akitazama. 4) Tena, akawatuma katika huduma ya muda mfupi (Mat. 10:1-11; Mk. 6:7-13; Luk. 9:1-6); anajadiliana matokeo pamoja nao hatimaye; 5) anawatuma peke yao (ijapokuwa, kama Bwana Mfufuka, bado yuko pamoja nao. Mat. 28:20). Kisha wanafunzi nao wakaanza kufanya vivyo hivyo kwa Wakristo wengine. Hivyo, mafunzo kuelekea kujitegemea ni kipengele kikuu katika umisheni.

Hoja 5: Jukumu muhimu kabisa la Yesu katika kipindi kati ya ufufuko na kupaa kwake huko mbinguni lilikuwa ni umisheni wa kiulimwengu.

Injili zote nne hujumuisha muundo fulani wa Agizo Kuu uliotolewa katika kipindi kilichofuata ufufuko (Mat. 28:16-20; Mk. 16:15-20; Luk. 24:13-53, hasa mistari ya 44-49; Yoh. 20:11-23, hasa mistari ya 21-23; Mdo. 1:4-11). Maagizo mbalimbali huonesha kuwa Yesu alitangaza umisheni wa kiulimwengu, akifanya uwezekane kwa kifo chake cha kidhabihu Msalabani, kwa mtazamo muhimu zaidi wa mateso yake, kifo chake na ufufuko wake.

Hoja 6: Pentekoste hudhihirisha kuwa umisheni wa kiulimwengu katika nguvu za Roho ni sifa muhimu zaidi ya kanisa la Kristo.

Mara kwa mara Yesu alikuwa amewaamuru wanafunzi wake kumsubiri Roho Mtakatifu kabla ya kuanza kuyahubiri injili mataifa ya ulimwengu (Mk. 16:15-20; Mdo. 1:4-11). Roho alikuwa aje ili auhakikishie ulimwengu Injili mahali pa Yesu (Yoh. 16:7-11). Kwa ujio wa Roho Mtakatifu, kanisa la Agano Jipya na umisheni wa kiulimwengu vilianza kwa pamoja. Kwenye siku ya Pentekoste, jinsi mitume walivyoanza kunena katika lugha za wasikilizaji kutoka sehemu mbalimbali za ulimwengu wote, na kwa jinsi ambavyo wasikilizaji walivyoweza kuwaelewa, ilikuwa dhahiri kuwa Injili iliwezekana kupitia nguvu za Roho Mtakatifu, kushinda vizingiti vyote vya kitamaduni na vya lugha.

Hoja 7: Bila Roho Mtakatifu, umisheni wote wa kiulimwengu na mikakati yote ya umisheni itakuwa ni bure na haitatimia.

Ni Roho Mtakatifu pekee awezaye kuwahakikishia watu hatia yao (Yoh. 16:7-10), kuwaongoza katika kumwelewa Mungu na wokovu kupitia kwa Yesu na kuwafanya viumbe wapya katika Kristo (Yoh. 3:5). Ijapokuwa Mungu huwaruhusu Wakristo kushiriki katika umisheni wa kiulimwengu na huwataka watumie akili zao ili kuwafikia wengine (kwa mfano, angalia mipango mingi ya akina Paulo na vile vile mkakati wake wa jumla, mf. katika Rum. 1+15), mikakati ya umisheni inaweza kuwa yenye mafanikio tu endapo Mungu ameamua mipango hiyo ifanikiwe (1 Kor. 12:4-6; Rum. 1:13).

Hoja 8: Yesu alitoa hakikisho la mafanikio katika umisheni wa kiulimwengu kama matokeo ya Ubwana wake usioonekana. Mafanikio ya umisheni wa kiulimwengu huthibitisha Ubwana wake.

Agizo Kuu la Yesu katika injili ya Mathayo huhalalisha umisheni wa kiulimwengu kwa hakika, "Nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani." (Mat. 28:18), na kwamba atakuwa pamoja na kanisa lake daima (Mat. 28:20). Hivyo, Agizo Kuu si kazi ya kufanya tu bali pia ni ahadi. Yesu mwenyewe ajitwika wajibu kwa kuyafuasa mataifa yote, kwa kuwa anasema, "nitalijenga kanisa langu; wala milango ya kuzimu haitalishinda" (Mat. 16:18).

Kitabu cha Ufunuo kwa kurudia hutangaza kuwa watu wa lugha na tamaduni zote watakuwepo miongoni mwa kusanyiko kubwa lisilo na idadi la waliokombolewa. "Nao waimba wimbo mpya wakisema, Wastahili wewe kukitwaa hicho kitabu na kuzifungua muhuri zake; kwa kuwa ulichinjwa, ukamnunulia Mungu kwa damu yako watu wa kila kabila na lugha na jamaa na taifa, ukawafanya kuwa ufalme na makuhani kwa Mungu wetu" (Ufu. 5:9-10. Pia angalia Ufu. 7:9; 10:11; 14:6).

Hoja 9: Kupanuka ni sifa ya Ufalme wa Mbinguni, kama inavyobainishwa wazi hasa katika ishara za kinabii katika Kitabu cha Danieli na katika mifano ya Yesu.

Ndoto ya Nebukadreza inaishia na jiwe linaloviringirika kutoka mbinguni na kuharibu sanamu ya falme, na kisha kuwa mlima mkubwa uliojaza dunia. Danieli anakiri, "Na katika siku za wafalme hao Mungu wa mbinguni atausimamisha ufalme ambao hautaangamizwa milele, wala watu wengine hawataachiwa enzi yake; bali utavunja falme hizi zote vipande vipande na kuziharibu, nao utasimama milele na milele" (Dan. 2:34-35, 44). Vile vile Danieli anaota juu ya falme zilizowasilishwa kama wanyama (Dan. 7:9-14, 26-27). Falme hizi zinafikia kikomo wakati Mwana wa Adamu, anayejulikana baadaye kwa jina la Yesu, anapaa mbinguni (Kupaa kwa Kristo), pindi apokeapo "mamlaka, na utukufu, na ufalme, ili watu wa kabila zote, na taifa zote, na lugha zote, wamtumikie;" (Dan. 7:14). Ufalme huu utakuwa ni wa milele (Dan. 7:14-27).

Ukweli wa mambo ni kuwa, Kristo aliujenga Ufalme wake, akianza na wanafunzi na Kanisa, katika kipindi cha Ufalme wa Rumi. Katika mifano mingi, Yesu alitabiri kuwa Ufalme wake utakuwa hadi utakapoijaza dunia yote (Kwa mfano, mfano wa magugu: Mat. 13:24-30, 36-43; mfano wa punje ya haradali: Mat. 13:31-32; mfano wa chachu: Mat. 13:33-35).

Ahadi ya ukuaji katika maagano yote ni ya kiulimwengu, ya ndani na ya nje, ya kiroho na ya idadi, kwa mtu binafsi na kwa kundi.

Ukuaji wa ndani na wa nje wa Ufalme wa Mbinguni na wa Kanisa la Yesu Kristo haumaanishi kuwa kila kanisa la Kikristo, dhehebu au kundi, hushiriki moja kwa moja katika upanukaji huu. Wakati mwingine Mungu huliadabisha Kanisa lake au huyaacha makanisa yasiyo maaminifu yafe (Ufu. 2:5; Rum. 11:20-21).

Hoja 10: Ukuaji na mafanikio ya mwisho ya Ufalme wa Mbinguni hauondoi, bali hujumuisha mateso ya Kanisa la Yesu Kristo. Ukristo hautoi kinga ya maisha yasiyo na matatizo.

Paulo si mwenye kiburi kwa sababu ya "**amani na Mungu**" kwa njia ya rehema ya Yesu Kristo (Rum. 5:1-2), bali anaandika: **"Nasi pia twafurahi katika mateso yetu, kwa sababu twajua kuwa mateso huleta uvumilivu … kwa sababu Mungu amemimina upendo wake ndani ya mioyo yetu kwa Roho Mtakatifu …"** (Rum. 5:3-5).

Mfano wa ngano na magugu (Mat. 13:24-30, 36-43), ambao huelezea ukuaji wa Ufalme wa Mungu, huonyesha kuwa si Ufalme wa Mungu tu utakaokua, bali pia na ufalme wa uovu. Hata hivyo, magugu yatadumu tu hadi ngano itakapokuwa tayari kwa mavuno. Uovu unaweza kukua tu kwa sababu Mungu analikuza kanisa lake. Kama hakungekuwa na kanisa ulimwenguni, ulimwengu ungekuwa tayari kwa ajili ya hukumu ya mwisho (Mwa. 18:22-23).

Hoja 11: Agano Jipya huhalalisha umisheni wa kiulimwengu, si hasa kwa Agizo Kuu, bali kwa nukuu kutoka Agano la Kale.

Katika kusoma mjadala wa Agano Jipya juu ya kuhalalisha umisheni wa kiulimwengu, mtu hugundua kuwa, takribani katika kila hali, Agano la Kale hunukuliwa badala ya Agizo Kuu, ambalo [yaani Agizo Kuu] lilikuwa ni ishara ya mwanzo kuwa, mpango wa Mungu ambao tayari ulikuwa umekwishatangazwa na ukaandaliwa, sasa ulipaswa kuendelea. Agizo Kuu ni utimizaji wa Agano la Kale. Kitabu chote cha Warumi, hasa Sura ya 15, ni mfano wa wazi kwa sababu Paulo ananukuu Agano la Kale daima katika waraka huu katika kutetea misheni.

Wakati Paulo na Barnaba walipokuwa wamekwishakataliwa na Wayahudi, na wao kutaka kuhalalisha uhubiri wa Injili kwa watu wa mataifa wa Antiokia, badala yake, hawakunukuu Agizo Kuu lililotolewa na Yesu, bali walinukuu Agizo Kuu kwa Isaya, "Kwa sababu ndivyo tulivyoamriwa na Bwana, Nimekuweka uwe nuru ya Mataifa, upate kuwa

wokovu hata nwisho wa dunia" (Mdo. 13:46-49, akinukuu Isa. 49:6). Muktadha wa mstari huu katika Isaya huonesha kuwa mitume walikuwa wakivutiwa na Agizo la Agano la Kale, "Ni neno dogo sana wewe kuwa mtumishi wangu ili kuziinua kabila za Yakobo, na kuwarejeza watu wa Israeli waliohifadhiwa; zaidi ya hayo nitakutoa uwe nuru ya mataifa, upate kuwa wokovu wangu hata miisho ya dunia".

Pia, Yakobo alihitimisha baraza la Yerusalemu kwa kuhalalisha mpango wa Paulo wa kuhubiri Injili kwa Mataifa kwa kutumia Amosi 9:11-12 (Linganisha Isa. 61:4, Zab. 22:27-28, Zek. 8:22), ambamo hekalu la Daudi – kwa Yakobo ni Kanisa – linajengwa upya kwa kuwaongeza Mataifa kwenye mabaki ya Yuda. Petro hutetea kuokolewa kwa Kornelio kwa rejea ya Agano la Kale, "Akatuagiza tuwahubiri watu na kushuhudia ya kuwa huyu ndiye aliyeamriwa na Mungu awe Mhukumu wa walio hai na wafu. Huyo manabii wote humshuhudia ya kwamba kwa jina lake kila amwaminiye atapata ondoleo la dhambi" (Mdo. 10:42-43).

Hoja 12: Uhalalishaji wa Agano la Kale kwa umisheni wa Agano Jipya hudhihirisha kuwa umisheni wa kiulimwengu ni mwendelezo wa moja kwa moja wa kazi ya Mungu tangu Anguko la Mwanadamu na uchaguzi wa Ibrahimu na kuendelea.

Yesu alithibitisha uhalalishaji wa Agano wa Kale kwa umisheni wa Agano Jipya katika Agizo Kuu la Luka. "Kisha akawaambia, Hayo ndiyo maneno yangu niliyowaambia nilipokuwa nikali pamoja nanyi, ya kwamba ni lazima yatimizwe yote niliyoandikiwa katika Torati ya Musa, na katika Manabii na Zaburi. Ndipo akawafunulia akili zao wapate kuelewa na maandiko. Akawaambia, Ndivyo ilivyoandikwa, kwamba Kristo atateswa na kufufuka siku ya tatu; na kwamba mataifa yote watahubiriwa kwa jina lake habari ya toba na ondoleo la dhambi, kuanza tangu Yerusalemu. Nanyi ndinyi mashahidi wa mambo haya." (Luk. 24:44-48). Kwa mujibu wa maneno haya, sehemu zote za Agano la Kale hazizungumzi tu juu ya ujio wake na juu ya Msalaba wake na Ufufuo wake, bali pia huelezea umisheni wa kiulimwengu: msamaha ni lazima uhubiriwe kwa mataifa yote.

Hoja 13: Uchaguaji (uteuaji) wa watu wa Agano la Kale ulifany-wa huku wazo la mataifa yote likitiliwa maanani, hivyo basi dha-mira ya umisheni wa kiulimwengu tayari ilikuwemo katika Agan-o la Kale.

Ibrahimu, Isaka na Yakobo waliteuliwa, ili mataifa yote dunia yapate kubarikiwa kupitia wao. (Mwa. 12:3; 18:18; 22:18; 26:4; 28:14). Hivyo

ahadi waliopewa mababu hawa inarejewa katika Agano Jipya kama halalisho la ufanyaji injili kwa watu wasio Wayahudi (Luk. 1:54-55, Mdo. 3:25-26, Rum. 4:13-25, Efe. 3:3-4, Gal. 3:7-9, 14, Ebr. 6:13-20, 11:12).

Hoja 14: Kwa sababu hii, Agano la Kale hujumuisha mifano mingi ya watu wasio Wayahudi waliosikia ujumbe wa Mungu kwa kupitia Wayahudi na kuipokea imani ya wokovu kwa Mungu mmoja wa kweli. Kwa wakati ule ule, vifungu vingi vya vitabu vya unabii katika Agano la Kale vinaelekezwa kwa mataifa ya kipagani.

Kwa mfano, Kitabu cha Ruthu kinaarifu kuhusu uongofu wa wapagani, Kitabu cha Yona huarifu juu ya safari ya kimishenari yenye mafanikio ya nabii huko Ninawi.

Takribani manabii wote wa Agano la Kale huyaita mataifa ya kipagani yatubu. Naamani wa Shamu, Yethro ambaye ni baba mkwe wa Musa na kahaba Rahabu ni mifano mitatu tu ya makafiri waliomgeukia Mungu aliye hai. Mara kwa mara, Agano la Kale limeandika matamko ya viongozi wa dunia ambayo yanamsifu Mungu na yanayoelekezwa kwa watu wote (zaidi sana katika Ezra, Nehemia, Esta na Danieli).

Hoja 15: Umisheni wa kiulimwengu hauwezi kutengwa na Agano la Kale, na historia ya watu wa Israeli na historia ya wokovu ya Agano la Kale lakini ni sharti ufanywe na kufasiliwa katika nuru ya mafundisho yake.

Paulo hulithibitisha hili katika Warumi 9-11. Uhusiano kati ya umisheni wa kiulimwengu na Wayahudi una pande mbili: kwanza, kuchaguliwa kwa Wayahudi, na pili, kutotii kwao, “Basi kwa habari ya Injili wamekuwa adui kwa ajili yenu; bali kwa habari ya kule kuchaguliwa wamekuwa wapenzi kwa ajili ya baba zetu” (Rum. 11:28). Paulo anaonyesha kuwa uongofu ujao wa Wayahudi kwa Masihi wao, Yesu Kristo, utakuwa na matokeo chanya yasiyo na kipimo juu ya ufanyaji injili kwa mataifa yote. (Rum. 11:15, 24-26).

Hoja 16: Kitabu cha Warumi huonesha kuwa umisheni wa kiulimwengu ni lazima ukite mizizi katika mafundisho ya Biblia yafaayo na yaliyo kamili, na hayo mafundisho ya Kibiblia pangilivu na daima huongoza kwenye umisheni wa kiulimwengu.

Paulo aliandika kitabu cha Warumi akiwa kwenye harakati za kazi ya umisheni na anahalalisha umuhimu wa utangazaji wa Injili ulimwenguni

mwote. Kwa wakati uleule, Kitabu cha Warumi ni wasilisho pangilivu la Kibiblia la Injili na tamko la imani ya Kikristo katika Biblia. Katika kitabu cha Warumi, Paulo anapanga kuja Rumi (Rum. 1:14-17), kwa sababu anataka kutangaza Injili kwa watu wote bila kizuizi, bila kujali lugha, utamaduni, ujamii ("Wayunani na wasio Wayunani"), elimu au madaraja ya kijamii ("wenye hekima na wasio na hekima"). Kwa kufuata maelezo haya ya mpango wake wa kimishenari, anaanza somo 'halisi'. Vifungu vyenye kujulikana sana vinavyotoa utangulizi wa mafundisho yake (Rum. 1:16-17), huanza na "Kwa maana …". Mwishoni mwa waraka wake (Rum. 15:14-16, 27) Paulo anaigeukia mipango yake halisi ya misheni. Sura zilizopo katikati ni uhalalishaji tu wa kidogma wa mipango yake. 'Utii wa imani' ni sharti udhamiriwe kwanza, ndipo unapoweza kutangazwa kwa mataifa yote.

Mtu yeyote anayeshiriki kwenye misheni kwa nguvu tu, bila kurejea kwenye 'mafundisho', hufanya hivyo kwa utukufu wa jina lake mwenyewe, kwa sababu anatupilia mbali maelekezo ya Mungu. Yeyote afundishaye 'mafundisho' bila ya kurejea kwenye umisheni, hufundisha mawazo yake mwenyewe na hutupilia mbali sababu zilizomfanya Mungu kutupa Neno lake.

Sehemu II: Umisheni na Tofauti za Kitamaduni

Hoja 17: Aina mbalimbali za watu na tamaduni si matokeo ya dhambi, bali ulikuwa ni mpango wa Mungu. Kwa mujibu wa Maandiko, tunahitaji kukataa tu vile vipengele vya kitamaduni ambavyo kwa uwazi huhitilafiana na mapenzi yake matakatifu.

Tofauti za kitamaduni si mbaya wala si matokeo ya hukumu ya Mungu kwa njia ya kuchafua lugha kufuatia ujenzi wa Mnara wa Babeli (Mwa. 11:1-9). Kwa kuchafua lugha za mwanadamu, Mungu alitekeleza amri yake mwenyewe, yaani kuwatawanya juu ya dunia yote ("mkaijaze nchi", Mwa. 1:28; 9:1), ambako moja kwa moja kulisababisha mgawanyiko wa wanadamu katika makundi ya kifamilia na ya mataifa; na vile vile ya taaluma, uwezo na tamaduni. Katika kujenga Mnara wa Babeli, mwanadamu alijaribu kujenga utamaduni wa kiulimwengu mmoja na unaofanana. Kama Kitabu cha Ufunuo na Mpinga Kristo katika Maagano yote mawili vinavyoweka wazi, daima huu umekuwa ni mpango wa Shetani. 'Mnyama' katika Ufunuo anapokea nguvu kutoka kwa 'Joka': "Tena akapewa kufanya vita … akapewa uwezo juu ya kila kabila na jamaa na lugha na taifa" (Ufu. 13:1-10). Hata hivyo, kamwe Mungu hataki mji mmoja unaofanana, serikali moja ya ulimwengu wote, wala mfumo wa

Ubinadamu unaofanana. Neno lake linahakikisha kuwepo kwa umoja wa ulimwengu, lakini si katika muundo wa kidunia unaoonekana. "Akatawanya" wanadamu "usoni pa nchi yote" (Mwa. 11:9).

Tangu kwa wana wa Nuhu na kuendelea "nchi yote ikaenea watu" (Mwa. 9:19) na watu, "**wakatawanyika … kwa kulingana na mataifa yao**" (Mwa. 10:5; 10:32). Kwa hiyo, Mungu ni mwumba wa utaifa wowote duniani kwa sababu "**kutoka kwa mtu mmoja alifanya kila taifa la wanadamu, ili waweze kuikalia dunia yote; na aliamuru nyakati zilizowekwa kwa ajili yao na mahali halisi pale wapaswapo kuishi**" (Mdo. 17:26; ni sawa na katika Kumb. 32:8, Zab. 74:17).

Hoja 18: Wakristo wako huru mbali na shinikizo lolote la kitamaduni. Hawahitajiki kukubali mapokeo au amri yoyote ya mwanadamu kando na zile zilizotolewa na Mungu.

Jambo hili liko wazi hasa katika Marko 7:1-13 pale Yesu anapowashutumu Mafarisayo kwa kuinua juu utamaduni wao wenyewe wa kibinadamu kwa kiwango sawa na Sheria ya Mungu.

Hoja 19: Wakristo wanaweza kuzitolea hukumu tamaduni nyingine kwa kulingana na vipimo vya Kibiblia, pindi wanapokuwa wamejifunza kutofautisha kati ya utamaduni wao wenyewe (na hata tamaduni zao wenyewe za Kikristo) na sheria zote halali za Mungu.

Marko 7:1-13 hulieleza vema jambo hili. Mafarisayo walikuwa na nia ya kiheshima na kitawa kwa kuunda kanuni za lazima ambazo ni nyongeza kwenye Sheria ya Mungu, ambapo nyingi ya sheria hizo, kihalisia zilihitilafiana na Sheria ya Mungu. Kwa ukali Yesu analishutumu kundi hilo kwa kulinganisha desturi zao wenyewe na Sheria ya kiungu: "**Wananitumikia bure, kwa sababu wanafundisha amri za wanadamu**" (Mk. 7:7; Mat. 15:9).

Hoja 20: Kwa sababu Wakristo wako kwa Kristo pekee na wanapaswa kujinyenyekeza chini ya Neno lake pekee, wanaweza kuzitazama tamaduni zao na zile za watu wengine kwa kuzihakiki, lakini wanatakiwa kwa upendo kuishi kwa kulingana na tamaduni za wengine.

Katika 1 Kor. 9:19-23, Paulo anaeleza umuhimu wa kuishi kwa kulingana na tamaduni za wengine wakati wa kufanya uinjilisti: "Maana, ingawa nimekuwa huru kwa watu wote, nalijifanya mtumwa wa wote, ili nipate

watu wengi zaidi. Nalikuwa kama Myahudi kwa Wayahudi, ili niwapate Wayahudi; kwa wale walio chini ya sheria, nalikuwa kama chini ya sheria, (ingawa mimi mwenyewe si chini ya sheria), ili niwapate walio chini ya sheria. Kwa wale wasio na sheria nalikuwa kama sina sheria, (si kwamba sina sheria mbele za Mungu, bali mwenye sheria mbele za Kristo), ili niwapate hao wasio na sheria. Kwa wanyonge nalikuwa mnyonge, ili niwapate wanyonge. Nimekuwa hali zote kwa watu wote, ili kwa njia zote nipate kuwaokoa watu. Nami nafanya mambo yote kwa ajili ya Injili ili kuishiriki pamoja na wengine."

Mkristo anaweza kujihusisha sana katika utamaduni wake mwenyewe, kiasi kwamba hatambui kuwa katika hali bora kabisa haeleweki na katika hali mbaya kabisa yeye ni "kikwazo" (1 Kor. 9:12) kwa wengine kuielewa Injili.

Hoja 21: Hatuhusiki tu na kuwaeleza watu wengine habari njema za wokovu kupitia kwa Yesu Kristo, bali pia kuhakikisha kuwa watu wameuelewa ujumbe.

Hii ndiyo sababu, ni kwa nini Biblia na Kurani zinaweza kutafsiriwa katika kila lugha na kwamba Injili iweze kutangazwa na ni sharti itangazwe katika kila muundo wa lahaja na utamaduni.

Hoja 22: Umisheni wa kiulimwengu haupuuzi hali za kijamii zilizopo, bali huzitumia kimkakati. Kwa sababu hii, Paulo alianzisha makanisa katika viunga vikuu vya kibiashara na vituo vyenye watu wengi, akiacha shughuli za uenezaji Injili kwa maeneo ya jirani kwa makanisa haya, na akaendeleza Injili katika maeneo ambayo hayakuwa yamefikiwa na kuanzisha makanisa mapya.

Kwa kawaida, Paulo alianzisha makanisa katika maeneo ya vituo vikubwa vya kitamaduni, kwa haraka akachagua wazee waliofundishwa na yeye kuongoza makanisa, na baadaye akaendelea, akiacha upenyezaji wa Injili kwenye maeneo ya jirani kwa kanisa jipya. Anawaandikia Wathesalonike, "Hata mkawa kielelezo kwa watu wote waaminio katika Makedonia, na katika Akaya. Maana kutoka kwenu neno la Mungu limevuma, si katika Makedonia na Akaya tu, ila na kila mahali imani yenu mliyo nayo kwa Mungu imeenea; hata hatuna haja sisi kunena lolote" (1 Thes. 1:7-8).

Paulo asemapo, "tangu Yerusalemu, na kando kando yake, mpaka Iliriko nimekwisha kuihubiri injili ya Kristo kwa utimilifu" (Rum. 15:19), hamaanishi kuwa amekwishatangaza Injili kwa kila mtu katika sehemu

hiyo, bali ni kwamba amefungua makanisa katika maeneo ya kimkakati. Jambo hili pia ni kweli kwa tamko kuwa hana wasaa tena katika maeneo haya (Rum. 15:23). Hatafuti maeneo ambayo Kristo amekwishatajwa tayari, wala maeneo ambayo wengine walikuwa wamekwishahubiri. (Rum. 15:20-21), bali maeneo ambayo hakuna mtu amekwishatangaza Injili na ambako hakukuwa na makanisa.

Hoja 23: Upendeleo wowote ule – uwe umetokana na hadhi ya kiutamaduni, ya kiuchumi au kwa sababu nyingine yoyote – huenda kinyume na tabia ya Mungu na imani ya Kikristo.

Kwa sababu Mungu hana upendeleo kabisa, Serikali na kanisa la Agano Jipya ni lazima visiwe na upendeleo (Kumb. 1:17; 10:17-18; 16:18-20; 2 Nya. 19:7; Mith. 18:5; 24:23; Ayu. 13:10, Kol. 3:25, Efe. 6:9; Yak. 2:1-12). Yakobo anaandika, "Ndugu zangu, msiishike imani ya Bwana wetu Yesu Kristo, Bwana wa utukufu, kwa upendeleo … Iwapo kweli mnatimiza sheria ya kifalme kwa kulingana na Maandiko, 'mpende jirani yako kama nafsi yako', mwafanya vema; lakini mkionesha upendeleo, mwafanya dhambi, na kuhukumiwa na sheria kuwa wakosaji … Hivyo semeni na fanyeni kama watu watakaohukumiwa kwa sheria ya uhuru" (Yak. 2:1, 8-9, 12).

Hoja 24: Majadiliano ni sifa adilifu ya Kikristo wakati imaanishapo majadiliano ya amani, uungwana, usikilizaji wenye ustahamilivu na kujifunza kutoka kwa wengine.

Majadiliano kati ya Wakristo waliothibitika na waumini wa dini nyingine yawezekana, mradi tu kama Wakristo wako radhi kuzungumza na wengine kwa amani juu ya imani yao ("Mwe tayari siku zote kumjibu kila mtu awaulizaye habari za tumaini lililo ndani yenu; lakini kwa upole na kwa hofu," (1 Pet 3:15) na kuwasikiliza wengine (Yak. 1:19). Wanatamani kujifunza kutoka kwenye uzoefu wa wengine katika nyanja nyingi za maisha (Angalia hasa Kitabu cha Mithali) na wana nia kujiuliza juu yao wenyewe na tabia zao.

Hoja 25: Majadiliano ambayo husalimisha tamko la Kikristo la kumiliki ukweli mkamilifu au yanayotupilia mbali umisheni wa kiulimwengu ni jambo lisilofikirika, kwa kuwa linautupilia mbali Ukristo wenyewe.

Majadiliano yanayomtaka Mkristo, kwa muda au kimsingi kuyaacha madai ya ukweli mkamilifu kumhusu Yesu Kristo (Yoh. 14:6), Injili (Rum. 1:16-17, 2:16) au Neno la Mungu (2 Tim. 3:16-17, Ebr. 4:12-13, Yoh. 17:17), kiasi kwamba ufunuo wa Kibiblia unalinganishwa na imani za dini nyingine, hauwezi kupatanishwa na umisheni wa Ukristo au na kiini cha Ukristo wenyewe.

Tamko la Kikristo la kumiliki mamlaka kamilifu liko juu ya yote yanayoelezwa katika mafundisho ya Hukumu ya Mwisho na Uzima wa Milele. Waebrania 6:1-2 huelezea "kufufuliwa wafu, na hukumu ya milele" kama vipengele viwili miongoni mwa sita vya imani yetu vilivyo muhimu, kama Tamko la Imani ya Mitume linavyosema, "kutoka huko atarudi kuhukumu walio hai na wafu".

Sehemu III: Kuongoka na Mabadiliko ya Kijamii

Hoja 26: Amani kati ya mtu na Mungu – wokovu binafsi kwa njia ya kifo cha kidhabihu cha rehema cha Yesu msalabani – ni lengo la kwanza kabisa la umisheni na sharti ambalo ni chimbuko la mengine yote.

Katika Mat. 16:26, Yesu alieleza wazi kuwa wokovu wa nafsi ni muhimu kuliko jambo lingine lolote: "Kwani atafaidiwa nini mtu akiupata ulimwengu wote, na kupata hasara ya nafsi yake? Au mtu atatoa nini badala ya nafsi yake?"

Katika Waraka kwa Warumi, Paulo kwa mfuatano anaelezea ni kwa nini Wayahudi na watu wa mataifa wamepotea katika dhambi, na kwa nini ni Yesu pekee ndiye awezaye kuleta wokovu. Warumi 5:1-2 inahitimisha, "**Kwa hiyo, tukiisha kuhesabiwa haki kwa imani, tuna amani na Mungu, kupitia kwa Bwana wetu Yesu Kristo, ambaye kwa kupitia yeye pia tuna kuifikia kwa njia ya imani neema hii ambayo kwayo tunasimama …**". Ni baada ya hayo tu, ndipo anageukia masuala ya kibinafsi, ya kijamii, ya kiutamaduni na ya maadili ya kisiasa.

Hoja 27: Kipaumbele cha lengo la wokovu wa mtu binafsi katika umisheni hakuondoi malengo mengine, bali huyapa malengo hayo umuhimu wake.

Agizo Kuu katika Mathayo 28:18-20 hujumuisha amri ya kuwafanya watu wote kuwa "wanafunzi" (wafuasi). Hatua ya kwanza ni kushawishika na kutubu kwa mtu binafsi. Ubatizo katika Jina la Utatu ni wa lazima kwa mtu mwenyewe. Hii ndiyo njia aitumiayo Mungu kuyapata 'mataifa' yote. Hivyo, lengo la kuongoa asilimia kubwa ya watu halipingani na hitaji la toba binafsi.

Uongofu hauashirii mwisho, bali mwanzo wa mtu kufanywa upya, vile vile na kufanywa upya kwa familia, kanisa, uchumi, serikali na jamii. Kila mtu ni lazima awe mwanafunzi ('mfuasi') wa Yesu Kristo. Katika ile amri ya kuwafunza "kuyashika yote niliyowaamuru ninyi", Agizo Kuu hujumuisha himizo la kufundisha maadili yote ya Biblia. Katika kumbadilisha mtu, maisha yake ya kila siku na mazingira yake, umisheni hushinda mifumo ya dhambi na dhuluma zinazoonekana.

Hoja 28: Huduma za kijamii ndani ya kanisa la Kikristo, hasa katika mtazamo wa tofauti za kiutamaduni, zilitaasisiwa tangu mwanzoni kabisa katika ofisi ya uhudumu.

Kuchaguliwa kwa wahudumu katika Matendo ya Mitume 6 na katika kanisa la Agano Jipya kwa ujumla ni jambo lenye umuhimu mkubwa. Inakubalika kuwa, kando ya ofisi za waangalizi (maaskofu) na wazee, ambao walihusika na uongozi na ufundishaji; kanisa lilikuwa na ofisi nyingine moja tu, ile ya wahudumu wa kiume (Flp. 1:1; 1 Tim. 3:8-13) na wahudumu wa kike (Rum. 16:1; 1 Tim. 3:11-13), ambao kwa asili kazi zao zilikuwa za kijamii. Wajibu wa kijamii wa kanisa kwa washiriki wake umetaasisiwa katika ofisi ya wahudumu, kiasi kwamba kanisa bila wao ni jambo lisilofikirika sawa na kanisa bila uongozi au mafundisho ya Biblia.

Kanisa lenyewe hujitwika kikamilifu wajibu wa kijamii kwa washiriki wake, endapo familia ya mtu mwenyewe haiwezi kufanya hivyo (1 Tim. 5:1-4). Kazi hii hujumuisha zaidi ya utoaji wa misaada au usaidizi kwa wachache, bali katika kuwajibika kwa wote.

Agizo katika Mathayo 25:45, kusaidia mdogo wa ndugu, linapaswa lieleweke katika maana hii. 'Ndugu' ni kaka na dada waaminio wa Yesu, na si yeyote yule. Ama sivyo, hiki kingekuwa kifungu pekee katika Agano Jipya kinachotumia neno 'ndugu' kimafumbo kurejea mtu yeyote kuliko washiriki wa kanisa na Wakristo wapendwa.

Hoja 29: Matendo 6 hutoa kipaumbele kikubwa kwa jukumu la kijamii la kanisa kwa washiriki wake, lakini wajibu wa kutangaza Neno la Mungu na maombi hubaki kuwa wenye umuhimu zaidi na umetaasisiwa katika ofisi ya wazee na mitume.

Mitume wanatoa sababu ifuatayo ya kukataa kulikubali "jambo" hili (Matendo 6:3), "na sisi tutadumu katika kuomba na kulihudumia lile Neno" (Matendo 6:4). Maombi na utangazaji wa Neno, vitu ambavyo huwa viko pamoja, vina kipaumbele kuliko kujihusisha na masuala ya kijamii na, ni mambo yasiyopaswa kutelekezwa. Mwunganiko wa maombi na mafundisho si jambo geni. Muda mrefu huko nyuma, ilikuwa ni huduma ya nabii Samweli na viongozi wengine wa Agano la Kale "kuomba" na "kufundisha" (1 Sam. 12:23).

Hoja 30: Wajibu wa kijamii wa Wakristo kwa ndugu zao ni sharti utofautishwe na wajibu wao wa kijamii kwa wengine.

Msaada wa kijamii kwa ndugu ni kazi iliyotaasisiwa katika ofisi ya wahudumu, ilhali huduma za kijamii hutolewa kwa wengine pindi inapowezekana na iwapo tu vitu au mali zipo. Kwa nyongeza, mtu aombaye msaada yeye mwenyewe asiwe chanzo cha uhitaji wake. "Usiwanyime watu mema yaliyo haki yao, ikiwa katika uwezo wa mkono wako kuyatenda" (Mith. 3:27). Wagalatia 6:10 huwapa changamoto waamini kuwahudumia watu wote, lakini husisitiza kipaumbele kipewe waumini wapendwa, "Kwa hiyo kadiri tupatavyo nafasi na tuwatendee watu wote mema; na hasa jamaa ya waaminio".

Kwa sababu Wakristo hunuia kuonesha upendo wa Mungu kwa maadui zao, na wanapaswa kuwabariki wale ambao huwalaani (Rum. 12:14), husaidia bila ubaguzi popote wawezapo. Wana nia ya kusaidia katika mazingira yenye uhitaji halisi, vile vile kufichua mifumo ya kijamii ya dhambi kwa kutumia Maandiko, na kuibadilisha pale inapowezekana, lakini bila kutumia nguvu.

Hoja 31: Kazi ya umisheni huanzia ndani ya kanisa na ndani ya familia ya Kikristo kwa kuwa kielelezo, kwa kupitia elimu na kwa kufundisha Neno la Mungu kwa kizazi kijacho.

Utangazaji wa Neno la Mungu kwa watu walio nje ya kanisa haupaswi kufanyika kwa gharama ya familia ya Kikristo. Familia nzuri ya Kikristo ni sifa ya msingi [inayotakiwa] kwa nafasi zote za uongozi katika kanisa la

Agano Jipya (1 Tim. 3:4-5, 12-13, Tit. 1:6-7). Pindi wazazi Wakristo wanapoacha ulezi wa watoto wao kwa wengine, wanaweza pia kupoteza uwezo wao wa kulishawishi Kanisa, Serikali, uchumi na jamii, kwa kuwa wameiacha njia bora zaidi ya kulifikia lengo hilo.

Kiambatanisho:

Rushwa na Ufisadi

Safari yetu ya kurudi kutoka mji mkuu la Indonesia uitwao Jakarta ilikuwa imeshaandaliwa vema, ikalipiwa na ikathibitishwa; lakini tulipokwenda kuhakikisha tulielezwa kuwa viti vyote vilikuwa vimejaa. Kulalama kwetu hakukufua dafu, hivyo basi ilibidi tusalie kwa wiki moja yenye karaha ya wakati wa msimu wa mvua huko Indonesia. Kwa matarajio mema, tuliweza kuishi na marafiki zetu Wakristo. Kila siku tulielezwa vile vile kuwa viti vyote vya ndege vimejaa. Hatimaye, shemeji yangu ambaye huishi katika nchi hii alitueleza tatizo: mnapoenda kwa utibitisho mtagundua kwamba kaunta ina sehemu mbili. Katika sehemu ya juu unaweka tiketi yako na halafu chini yake unaweka zawadi. Baada ya kufanya hivyo tulipata viti vyetu mara moja. Wafanyakazi katika kaunta hizi hulipwa mshahara duni, kwa sababu serikali hufikiri kuwa kwa hali ya kawaida watajiongezea pato kwa kupokea rushwa – dhamana ya mzunguko usioisha.

Hayo yalitukia miaka kumi na mitano iliyopita na tulifurahi kurudi katika nchi yenye "kuaminika" ya Ujerumani. Lakini makala-pendwa na kesi nyingi za kisheria zinafichua kuwa rushwa na ufisadi vinaongezeka hapa, katika masuala madogo madogo kama mfano wetu ulivyo na hata katika masuala makubwa. Ukansela wa Rainer Barzel uliangushwa kwa kura mbili, kwa sababu wajumbe hao walikuwa wamenunuliwa na Ujerumani Mashariki – Kuanguka kwa ukuta wa Berlin kulifichua jambo hili. Mambo tuliyozoea kuyasikia kutoka katika Ulimwengu wa Tatu au kutoka katika nchi ya Italia yanaanza kuwa mambo ya kawaida, mambo ya kila siku. Iliyopata kuwa njozi rasmi isiyoharibika ya nidhamu ya Prussia [dola ya kale ya Kijerumani], inapotelea mbali. Ijapokuwa mahakama inaonekana kuziachilia mbali kesi za rushwa, upakaji mafuta [rushwa] unaongezeka miongoni mwa maofisa wa polisi, maofisa wa ushuru, watumishi wa umma na maofisa wa taasisi za usimamizi. Ni wachache wanaoelewa kuwa jambo hili ni matokeo ya kuuacha kwetu Ukristo. "**Mtu mwovu hupokea rushwa nyuma mgongoni kupotosha njia za haki**". (Mith. 17:23) Yeyote anayemkataa Mungu wa Kikristo anayaacha mapenzi ya hakimu wake mkuu, ambaye haki yake kamilifu na ukosefu wa ufisadi kwake ndipo mahali pa ukanaji wa kila ukiukwaji wa haki kwa sababu ya tamaa ya fedha au ya mamlaka, kwa kuwa Mungu wa Agano la Kale mara kwa mara huelezewa kuwa asiye na upendeleo, kama "**Mungu mkuu,**

mwenye uweza, na wa kuogofya, ambaye hajali nafsi za watu, wala kuchukua zawadi" (Kumb. 10:17) **"Kwa kuwa hakuna uovu kwa BWANA Mungu wetu, wala kuheshimu nafsi za watu, wala kupokea zawadi"** (2 Nyak. 19:7).

Majaribu ya Yesu katika Agano Jipya ni mfano sahihi. Ilimbidi authibitishe uadilifu wake mwanzoni tu mwa huduma yake. Si mkate wala mamlaka ambayo yangeweza kumfanya apokee rushwa. Hata Mwovu alipomwahidi mamlaka yote juu ya falme zote za dunia – rushwa kubwa kuwahi kutolewa – Yesu hakushawishika kwa mamlaka wala utajiri, bali alitii mapenzi ya Baba yake aliye Mbinguni. Alijitiisha kwa Mungu na si kwa matamanio yake.

Hili laonyesha kuwa, Biblia haichukulii suala la rushwa, ufisadi na ukiukwaji wa haki kama suala dogo bali kubwa sana. Dhamira ya ufisadi hudhihirisha jinsi ambavyo dhambi ndogo za kibinafsi na za kijamii zinavyoweza kutenganishwa. Ufisadi kwa kawaida huhusisha watu binafsi lakini ni uovu ambao pia huhusisha mifumo yote miovu, na ambayo inaweza kuharibu jamii yote nzima; kwa kuwa viongozi wa nyanja zote za jamii – yaani Kanisa, uchumi na serikali – huangamizwa na huo ufisadi.

Katika lugha ya Kiebrania, mzizi wa neno tunaoutafsiri kama 'rushwa' humaanisha 'uharibifu'. Neno 'ufisadi' humaanisha 'uharibifu' au 'uteketezaji'. Si kwa bahati Biblia ya Kitaliano kutumia neno 'corruptio' (uteketezaji) kwenye dhambi ya asili, kwa kuwa Adamu na Hawa walishawishiwa na tumaini la mamlaka na maarifa ("Mtakuwa kama Mungu") na wakaasi.

Pengine, hakuna andiko jingine linaloeleza jinsi ufisadi unavyoharibu nyanja zote za maisha na jinsi unavyoharibu jamii kuanzia juu, kuliko shutuma itolewayo na nabii Mika: "**Mtawala aomba zawadi, hakimu anatafuta rushwa, na mtu mkuu anatamka matakwa yake maovu, hivyo wanapanga pamoja**" (Mika 7:3). "Mkono mmoja huuosha ule mwingine" hadi jamii inakamatwa na zimwi [la ufisadi] ambalo mkono wake ukikatwa unakua kwa haraka tena.

Mara tofauti kati ya uongo na ufisadi itakapokuwa imekwishaondolewa katika taasisi zenye mamlaka, Kanisa na watu wa Mungu hawawezi kukwepa kwa kuwa wameonesha upendeleo na wameshindwa kuzungumza hadharani dhidi ya ufisadi na tamaa. Mika anaonesha makosa ya viongozi wa Israeli, "**Wakuu wake huhukumu ili wapate rushwa, na makuhani wake hufundisha ili wapate malipo, na manabii wake hubashiri ili wapate fedha**" (Mika 3:11).

Unabii Zaidi Dhidi ya Ufisadi

Isaya 1:23, "**Watawala wako [ni] waasi, na marafiki wa wezi; kila mmoja hupenda rushwa, na hutafuta zawadi. Hawawalindi wasio na baba, wala mashtaka ya mjane hayafiki mbele zao.**"

Isaya 5:23, "**Wanaomhalalisha mwovu kwa rushwa, na kumwondolea mwenye haki haki yake!**"

Amosi 5:12, "**Maana mimi najua wingi wa dhambi zenu, na ukubwa wa dhambi zenu; mkiwaonea wenye haki [na] kuchukua rushwa; na kuwageuza maskini mlangoni [wasipate haki].**"

Si kwamba Agano la Kale au Agano Jipya hupinga zawadi, wakati zinapotoa msaada au kuletea furaha kwa wengine. Maandiko yanatambua kuwa zawadi ni kitu muhimu kwa ajili ya mafanikio ya malengo yaliyohalalishwa. Mithali husema, "Zawadi ya mtu humpatia nafasi; humleta mbele ya watu wakuu." (Mith. 18:16), na "**Zawadi ya siri hutuliza hasira; na tuzo kifuani humaliza ghadhabu kali**" (Mith. 21:14). Wakati Mkristo anakabiliwa na maofisa wafisadi na hana nafasi ya kukwepa ufisadi wakati huo, anaweza kuwa huru kujipatia haki yake kwa kutoa zawadi (kama tulivyofanya huko Indonesia). Ni pale tu anaponunua manufaa ambayo hakustahili ndipo anapokuwa mwenye hatia. Lakini, hata Mkristo anayelazimishwa kulipa ataupiga vita ufisadi na kuanza kwa kufichua na kwa kuondoa mifumo yote ya rushwa na ufisadi Kanisani.

Vifungu Vingine Dhidi ya Ufisadi na Rushwa

Kut. 23:8, "Na msichukue rushwa kwa maana rushwa hupofusha ufahamu na hupotosha maneno ya mwenye haki."

Kumb. 16:19, "Msipotoshe haki; msioneshe upendeleo; wala kuchukua rushwa; kwa maana rushwa hupofusha macho ya wenye hekima, na hupindisha maneno ya wenye haki."

Kumb. 27:25, "Amelaaniwa mtu yule achukuaye rushwa kumwangamiza mtu asiye hatia."

Zab. 15:5 inamsifu mtu ambaye "hachukui rushwa dhidi ya mtu asiye hatia".

Mith 25:27, "Yeye aliye na tamaa kwa ajili ya faida, huisumbua nyumba yake mwenyewe, lakini yeye aichukiaye rushwa ataishi."

Mhu. 7:7 "Hakika uonevu huharibu fikra za mtu mwenye hekima, na rushwa hudunisha moyo".

Isa. 33:15 "Ni yeye aendaye kwa haki, anenaye maneno ya adili; ni yeye anayedharau faida ipatikanayo kwa dhuluma; akung'utaye mikono yake asipokee rushwa".

Habari Kuhusu Mwandishi

Mwandishi

Thomas Schirrmacher ni mwenyekiti wa Theolojia ya Elimu-maadili, umisheni na Dini za kiulimwengu, ni Rais wa Martin Bucer Theological Seminary na Rais wa Gebende Haende gGmbH (Giving Hands = 'Mikono Itoayo') ambalo ni shirika hai la kimataifa la misaada; na vile vile mmiliki wa shirika la uchapaji na mmiliki mdau wa shirika la ushauri. Schirrmacher alizaliwa mwaka 1960, alisoma theolojia kuanzia mwaka 1978 hadi 1982 huko STH Basel na tangu mwaka 1983 alisomea Anthopolojia ya Utamaduni, na Ulinganifu wa Dini katika Bonn State University. Alitunukiwa Shahada ya Uzamivu wa Theolojia katika Misheni huko Johannes Calvin Foundation (Kampen/Netherlands) mwaka 1985, Shahada ya Uzamivu wa Falsafa katika Anthropolojia ya Utamaduni huko Pacific Western University, Los Angeles (CA) mwaka 1989 na Shahada ya Uzamivu wa Theolojia katika Elimu-maadili huko Whitefield Theological Seminary, Lakeland (FL) mwaka 1996. Katika mwaka 1997 alitunukiwa shahada ya heshima ya Uzamivu (D.D) kutoka Cranmer Theological House.

Alikuwa mchungaji wa Ushirika wa Kiinjili wa Ujerumani (Evangelical Society of Germany) huko Bonn na Erftstadt mwaka 1982 hadi 1986, mchungaji mdau wa Kanisa Huru la Kiinjili (Evangelical Free Church) huko Bonn mwaka 1992 hadi 1998 na mchungaji wa Free Reformed Church huko Bonn mwaka 1998 hadi 2000.

Schirrmacher alifundisha Umisheni, Dini za Kiulimwengu na Anthropolojia ya Utamaduni huko FTA Giessen (Ujerumani) kutoka mwaka 1983 hadi 1989, na kutoka mwaka 1990-1996 alifundisha Elimu-maadili, Umisheni, Ulinganifu wa Dini na Anthropolojia ya Utamaduni huko 'Independent Theological Seminary' mjini Basel ('Staatsunabhaengige Theologische Hochschule Basel'-STH Basel). Alishikilia na anashikilia viti mbali mbali vya uprofesa, kwa mfano 1994-1999 'Philadelphia Theological Seminary' (PA, USA) (Umisheni), 1995-2000 huko Cranmer Theological House (Shreveport, LA) (Umisheni na Elimu-maadili), na tangu 1996 huko Whitefield Theological Seminary (Lakeland, FL) (Theolojia Pangilivu na Apolojetiki). Hutoa mihadhara au hufanya kazi katika shule mbalimbali kama Freie Theologische Akademie (Giessen, Theolojia Pangilivu), The Neues Leben Seminar (Altenkirchen, Theolojia Pangilivu), the Akademie fur Christliche Fuehrungskrafte

(Grummersbach, Elimu-maadili ya Kibiashara) na UNISA (University of South Africa).

Mbali na hayo anajihusisha sana kimataifa na elimu ya kiwango cha zaidi ya shahada ya kwanza ya masafa na ya tovuti, mfano, yeye ni mhusika mkuu wa Elimu ya Kitheolojia ya Ujerumani (Germany Theological Education) kwa njia Enezi ('Theologischer Fernunterricht des Neues Leben-Seminars' au the European Extension of Whitefield Theological Seminary). Pia anahusika katika shughuli zote mbalimbali za uchapaji. Amekuwa mhariri wa 'Bibel und Germeinde' kwa miaka kumi, sasa ni mhariri wa 'Evangelikale Missiologie', mhariri mdau wa 'Contra Mundum: A Reformed Cultural Review', mhariri wa 'Reflection: An International Reformed Review of Missiology' na Querschnitte. Ameandika na kuhariri vitabu 49 juu ya Elimu-maadili, Umisheni na Anthropolojia ya Utamaduni.

Tangu 1986 anamiliki shirika la uchapaji liitwalo 'Cultural and Science Publ.' (Verlag fuer Kultur und Winnsenschaft), ambalo huchapa vitabu vya kisayansi juu ya lugha, desturi, dini na umisheni. Ni mmiliki mdau wa Consulting Schirrmacher GbR, shirika la kibiashara na biashara ya elimu. Anatajwa katika Marquis "Who's Who in the World", katika "International Who is Who of Professionals", katika "Who is Who in der Bundesrepublik Deutschland" na katika "International Who's Who in Distance Learning".

Amemwoa mtaalamu wa Uislamu Dk. Christine Schirrmacher, Mkurugenzi wa Islam Insitute of the Lausanne Movement, Ujerumani. Ni profesa azungukaye wa Masomo ya Uislamu huko "Whitefield Theological Seminary" (USA), na mwandishi wa vitabu viwili bora vya Utambulishi wa Uislamu. Wanandoa hawa wana watoto wawili wadogo.